


**ACT**-Wazalendo yakunwa serikali Kutenga bajeti mchakato Katiba mpya

UKURASA 4




NIPASHE JUMATATU MACHI 27, 2023

Nipashe **Spotika**

WANASOKA WA5 WANAOFANANA KIUCHEZAJI NA RONALDO UK. 12-13

ARSENAL

KLABU 4 ULAYA ZENYE KIWANGO CHA KUSHANGAZA MSIMU HUU

**LONDON,** England

MSIMU wa soka wa 2022-23 umekuwa wa kushangaza na mabadiliko yasiyotarajiwa katika kila ligi.

Wakati baadhi ya timu za soka zimetimiza matarajio yao kabla ya msimu mpya, zimevuka muda wote na zinang'aa zaidi kuliko hapo awali. Timu hizi zimewachanganya wakosoaji na kuweka mazingira ya kumaliza msimu wa kusisimua.

Katika haya, tunaangalia kwa karibu timu nne bora ambazo zimekuwa na uwezo wa kustajabisha msimu huu hadi katikati ya Machi 2023...

**#4 Newcastle United**

Mnamo mwaka 2017, Newcastle United ilipandishwa daraja na kurejea Ligi Kuu Engand baada ya mwaka mmoja kutokuwapo kwa kushuka daraja. Klabu imeonesha maendeleo makubwa katika nyanja ya michezo na kiuchumi.

Kutokana na mauzo ya klabu hiyo kwa Waarabu, matokeo chanya kuonekana msimu huu kuwa wazuri kwa kiwango cha Ligi Kuu England.

Wachezaji kadhaa muhimu wametoa uchezaji bora, haswa katika safu ya ulinzi. Ukiangalia jedwali la sasa la Ligi Kuu England, Newcastle wameshinda michezo 12, sare 11, wamepoteza tatu na wameruhusu mabao 19 pekee, idadi ndogo zaidi kwenye ligi.

Kwa sasa wanashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi na wako mbioni kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao. Wanaweza hata kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa timu mbili zilizo juu yao zitateleza.

**#3 Napoli**

Katika hatua hii ya Ligi Kuu Italia, Serie A, Napoli ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa. Timu hiyo iko mbele ya Lazio iliyo nafasi ya pili kwa pointi 19.

Kwa maana jinsi Napoli wamekuwa wazuri msimu mzima, hakuna uwezekano wa kushuka kwa uongozi wao hivi karibuni. Wachezaji kama Osimhen, Kvaratskhelia, Zielinski na Anguissa wameongoza safu ambayo imeifanya Napoli kuwa kileleni mwa Serie A.

Hakuna aliyeona hili likija kwani Napoli ilikuwa timu ya juu ya wastani kwa muongo mmoja uliopita. Kwa kweli, wameshinda Serie A mara mbili tu mwaka 1987 na 1990 wakati Diego Maradona akiwa anawachezea. Kwa sasa wako kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#2 Arsenal**

Kila shabiki wa Arsenal amekuwa akingojea wakati huu kwa miaka mingi. Klabu hiyo ya London Kaskazini ilipata enzi yao yenye mafanikio zaidi miaka ya 2000 chini ya Arsene Wenger.

Tangu walipotwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mwaka 2004 bila kupoteza, kombe hilo halijawafikia tena. Hadi sasa wameweza kushinda Kombe la FA na Ngao ya Jamii na wametolewa kwenye Ligi ya Europa.

Arsenal wamedumisha subira kwa kocha wa sasa, Mikel Arteta na wameanza mavuno ya matunda ya klabu kwa ufanisi. Wanapewa nafasi kubwa ya kushinda taji la Ligi Kuu baada ya takribani miaka 20.

Uchezaji wao msimu huu umekuwa wa kustaajabisha, ikiwa ni pamoja na ushindi wa dakika za majeruhi. Hata hivyo, wakosoaji wengine bado wanawaita "Tembo walioketi kwenye tawi la mti", wakiwa na maana wanatarajia kuona wakianza kupata matokeo mabaya hivi karibuni.

**#1. Union Berlin**

Huenda wengi hawajaona maendeleo yao, lakini Union Berlin imekuwa ya kusisimua kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Timu hiyo inatukumbusha mafanikio ambayo Leicester City ilipata miaka miwili baada ya kupandishwa daraja hadi Ligi Kuu England.

Union Berlin kwa sasa ipo katika nafasi nne za juu za Bundesliga na imekuwa ikionesha uwezo wa hali ya juu. Kati ya 2009 na 2019, timu hiyo ilishiriki kwenye daraja la pili la soka Ujerumani.

Lakini mwaka 2019, Union ilikamilisha kazi ya kihistoria kwa kupata kiwango na kupanda Ligi Kuu.

Mnamo 2022, walifuzu kwa Ligi ya Europa League matarajio yanaongezeka kwani wengine wanatarajia kuendelea kujiondoa na hata kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**ISIKUPITE**

Erling Haaland ni kama yupo dunia yake mwenyewe ya soka. Kabla ya mapumziko ya Kalenda ya Fifa, amefunga mabao nane katika mechi mbili, lakini kwa msimu huu ameshatupia hat-trick sita huku akiwa na jumla ya mabao 42 aliyoifungia Manchester City hadi sasa msimu huu katika mashindano yote.


# Nipashe

Jumatatu Machi 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581262

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII


an digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11



# PM: Tunashusha riba mikopo benki

• **Asema** serikali imeshakaa na taasisi za fedha... *Ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**ZAIDI WATOTO 170 WAPATA MSAADA BIMA YA AFYA**

SHIRIKA la RHSC linalohudumia jamii inayoishi katika mazingira magumu hususani watu wenye ulemavu, limetoa msaada wa...

**UKURASA WA 4**

**TAA KUBORESHA VIWANJA VYA NDEGE KUVUTIA WAWEKEZAJI**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mussa Mbura, amesema wataendelea...

**UKURASA WA 7**

**WENYE DALILI TB WATAKIWA KUWAHI VITUO VYA AFYA**

WANANCHI Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi wametakiwa kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya...


## Auawa siku moja baada kutoka gerezani kwa dhamana

UKURASA 2




Mwenyekiti wa Nyumba Ali, Zawadi Msigala (kulia), ambaye ni mwanaharakati wa kutetea haki za wenye ulemavu Tanzania, akimkabidhi kitabu kinachohusu maisha yake, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, Dk. Rita Kabati, kwenye hafla ya Mtoto Bima Day ya kukabidhi kadi 172 za bima ya afya kwa watoto wenye ulemavu hivi karibuni mjini Iringa. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Madaktari bingwa wapelekwa Kagera kutibu Marburg

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA NA REKODI YA MIAKA 28 ROBO CAF** UK.14 **KATUNI** UK.6

# Madaktari bingwa wapelekwa Kagera kutibu ugonjwa Marburg

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

SERIKALI imeongeza madaktari bingwa sita katika Mkoa wa Kagera kuendelea kutoa huduma ya matibabu kwa wagonjwa watatu wanaoendelea na matibabu baada ya kuambukizwa ugonjwa wa Marburg.

Taarifa hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki mkoani hapo na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, (pichani) wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwendelezo wa utoaji huduma ya afya kuhusu ugonjwa huo, namna ya kukabiliana nao.

Ummy alisema lengo la kuongeza madaktari hao ni kutaka kusaidiana na madaktari waliopo mkoani humo katika kuhakikisha ugonjwa huo hausambai kwenda kwa jamii.

Alisema kuwa madaktari hao wametoka katika vitengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mbobezi wa magonjwa ya figo, wauguzi waliopata mafunzo maalumu ya wagonjwa mahututi na mbobezi wa magonjwa ya ndani.

" Marburg ni ugonjwa unaopaswa kufuatiliwa na kutolewa taarifa kwa ukaribu na haraka kwenye Shirika la Afya Duniani kwa kuzingatia kanuni za afya za mwaka 2003, hivyo tunaendelea kujitahidi kuudhibiti," alisema.

"Wananchi toeni taarifa kwa mgonjwa yeyote mtakayemwona ana dalili za ugonjwa huu."

Alisema kwa muda wa siku tisa tangu ugonjwa huo umeripotiwa kutoka Kata ya Maruku na Kanyangereko Halmashauri ya Bukoba, timu ya wataalamu



ilianza ufuatiliaji kwenye jamii.

Waziri Ummy alisema hadi sasa tayari wahisiwa 205 wamewekwa katika uangalizi wa karibu kwa sababu wametoka kwenye makundi ya familia ambazo zilikuwa zikiuguza wagonjwa.

"Hawa watu hawana ugonjwa wowote ila tumewashikilia ili kuwalinda na kulinda wengine endapo hawa watapata ugonjwa usisambae kwa wengine," alisema.

Alifafanua kuwa Wizara ya Afya itatoa ajira 1,322 za muda mfupi (miezi mitatu) na kila halmashauri kuwa na watoa huduma ngazi ya jamii, vijiji, vitongoji na kata.

Waziri Ummy alisema lengo ni kutoa elimu kwa wananchi wazingatie hatua za kitaalam na jinsi ya kujilinda na ugonjwa huo huku wakiendelea na shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Pia, alisema kuwa timu mbalimbali zitaendelea kugawanyika kwenda visiwani kutembelea maeneo hayo na kuangalia wananchi wenye dalili za ugonjwa huo.

# Majaliwa: Tunashusha riba mikopo ya benki

**Na Mwandishi Wetu,**
BARIADI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imeshakaa na taasisi za fedha nchini ili kujadili namna taasisi hizo zinavyoweza kupunguza viwango vya riba na makato mengine kwa lengo la kuwavutia wananchi wengi zaidi kunufaika na huduma zinazotolewa na taasisi hizo ikiwamo upatikanaji wa mikopo.

Majaliwa alibainisha hatua hiyo wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa tawi jipya la Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) Mkoa wa Simiyu iliyofanyika mkoani hapo mwishoni mwa wiki na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi waandamizi wa chama na serikali.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema hatua hiyo ya serikali imekuja ikiwa ni suluhisho baada ya kubaini kwamba kuna idadi kubwa ya wananchi wanaokwepa kutumia huduma rasmi za kibenki kwa kuhofia ukubwa wa viwango vya riba vinavyotozwa na taasisi hizo na makato mengine.

"Habari njema ni kwamba tumeshakaa na taasisi hizi za kifedha ikiwamo benki hii pendwa ya NBC na tayari wameshaanza kuchukua hatua kadri inavyowezekana.

"Kwa hiyo, hakuna haja ya kuhofia kuhusu hilo, mambo yanakwenda vizuri na NBC wamekuja hapa wakiwa na suluhisho la changamoto zenu ikiwamo mikopo ya biashara, kilimo na ufugaji, hivyo watumieni vizuri, wapo hapa kuwasaidia," alisema. Waziri Mkuu pia aliitaka benki hiyo kuhakikisha inafungua zaidi fursa za kiuzalishaji na ukuaji wa uchumi mkoani hapa hususani kupitia sekta za biashara, kilimo na ufugaji.

"Mkurugenzi wa NBC pamoja na menejimenti yako mmefanya kazi nzuri sana kuleta huduma zenu mkoani Simiyu. Huu ni mkoa unaoongoza kwa uzalishaji wa pamba nchini huku pia wakazi wake wakijihusisha na shughuli za biashara na ufugaji.

"Ila kwa muda mrefu wakazi hawa wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya mitaji kwa ajili ya shughuli zao. Nimefurahi kusikia kwamba NBC mmekuja mkiwa na nia ya kumaliza changamoto hiyo... hongereni sana," alipongeza.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, ujio wa benki hiyo mkoani hapa umefanyika wakati mwafaka kwa kuwa serikali imejipanga kukabiliana na changamoto zinazokwamisha ukuaji na uendeshaji wa biashara, akibainisha kuwa licha ya uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo uboreshwaji wa barabara kuu na kituo kikubwa cha mabasi, bado kasi ya ukuaji wa biashara hairidhishi huku kituo hicho kikiwa hakitumiki licha ya kugharimu Shilingi bilioni saba.

Awali akizungumzia tawi hilo jipya, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema hatua hiyo inalenga kupanua wigo wa benki hiyo kutoa huduma zake kwenye mikoa yote ya Tanzania ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kuwajumuisha Watanzania wengi zaidi kwenye mfumo rasmi wa fedha.

"Mkoa wa Simiyu ni kiungo muhimu sana katika uchumi wa Kanda ya Ziwa na taifa zima kwa ujumla. Hivyo, kuwapo wa mfumo rasmi wa kibenki, kupitia tawi hili la Benki ya NBC hapa Bariadi, kutasaidia sana kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kufungua fursa mpya za kifedha.

"Hapo awali, wateja wetu walikuwa wakipata huduma kupitia mtandao wetu wa wakala ambapo hapa Simiyu tuna zaidi ya mawakala 30," alisema.

Sabi alibainisha kuwa benki hiyo iko tayari kuhudumia makundi yote ya jamii zikiwamo taasisi za serikali, watumishi wa serikali, wafanyabiashara na wanafunzi.

"Sambamba na hilo, tawi hili pia linakusanya maduhuli ya serikali kupitia Mfumo wa Ukusanyaji wa Fedha za Umma (GePG) na kodi kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hivyo, ninawaomba sana wananchi wa Mkoa wa Simiyu na maeneo ya jirani kulitumia vyema tawi hili ili kujiletea maendeleo ya kiuchumi," alihimiza.

Ikiwa ni benki ya tatu kwa ukubwa nchini ikiwa inamiliki mali (assets) zenye thamani ya Sh. trilioni 1.52 na amana (deposits) zenye thamani ya Sh. trilioni 1.96 na wafanyakazi wapatao 977, Benki ya NBC inajivunia mtandao mkubwa wa huduma unaojumuisha matawi 48, mashine za kutolea fedha (ATM) 180, NBC Wakala zaidi ya 9,000 huku ikiwa imewekeza zaidi huduma zake kupitia simu za mikononi "NBC Kiganjani" na huduma za mtandao wa intaneti.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
25/03/2023

**TAARIFA KWA UMMA.**

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya jumatatu tarehe **27/03/2023** Kampuni ya **TRANSCONNECT LOGISTICS T LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka **Dar es salaam** kuelekea **Tunduma kupitia Mikumi.**

Gari yenye namba zifuatazo:
**T363DEY / T509AZF**

**VIPIMO**

Urefu - 17.40m
Upana - 4.74m,
kimo - 4.65m

Gari litasafirisha mzigo kuanzia saa12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

217341302


# Auawa siku moja baada ya kutoka gerezani

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATU wawili akiwamo David Deogratius (32) aliyeachiwa kwa dhamana siku moja baada ya kutoka Gereza Kuu la Butimba kwa tuhuma za wizi wameuawa na wananchi wakitekeleza tukio la wizi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, alisema baada ya Jeshi la Polisi kupokea taarifa za watu hao kushambuliwa, walifika eneo la tukio na kuwachukua kisha kuwapeleka katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, walifariki dunia wakipatiwa matibabu.

"Machi 24 majira ya mchana wananchi walimkamata David Deogratius na kumshambulia kwa silaha za jadi na kumsababishia kifo baada ya kumkuta akiwa amevunja nyumba ya Octavius Eustace, Mwalimu wa Shule ya Msingi Kirumba na mkazi wa Ihila 'A' kwa kupitia dirishani na kuiba televisheni aina ya Sumsung," alisema Kamanda Mutafungwa.

Aliongeza kuwa baada ya kupitia kumbukumbu za kiuhalifu walibaini kwamba David alitoka Gereza la Butimba Machi 22, mwaka huu kwa dhamana na kosa lake ni wizi.

Kamanda Mutafungwa alisema katika tukio lingine kijana Hakimu Joseph aliuawa na wananchi baada ya kushambuliwa kwa mawe wakati akitekeleza tukio la wizi.

Alisema wananchi walimkuta Hakimu akikata bati la nyumba kisha kuingia kwenye duka la kuuza pembejeo za kilimo linalomilikiwa na mfanyabiashara, Aziza Sadick na kuiba Sh. 600,000 pamoja na simu ndogo.

Aidha, alisema mtuhumiwa huyo wakati anatoboa ukuta, Baraka Segeno ambaye alikuwa ndani ya duka hilo akifanya mahesabu alisikia kishindo na kutoa taarifa kwa majirani walifika eneo hilo kwa wakati.

Kamanda Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo aliposikia watu wapo nje alipita kwenye tundu la bati lililokata na kuanza kukimbia kwenye paa la nyumba hiyo kwa lengo la kukwepa kukamatwa hali iliyofanya wananchi hao kuanza kumshambulia kwa mawe na kusababisha umauti.

**HABARI KITAIFA**

# Bil.1/- yatengwa kwa watafiti watakaochapisha kimataifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imezindua tuzo ya umahiri kwa watafiti kutoka taasisi za elimu ya juu za umma na binafsi nchini wanaochapisha matokeo ya utafiti katika majarida yenye hadhi ya kimataifa.

Matokeo hayo ya utafiti ni yale yanayoakisi na kujibu kero mbalimbali za kijamii na kiuchumi na yenye hadhi ya kimataifa na kila chapisho litakalokidhi vigezo na kushinda litapata cheti na Sh. milioni 50.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema serikali imeanzisha tuzo hiyo ili kuweka msukumo wa wahadhiri baada ya kuona wanaelekeza nguvu kwenye kufundisha pekee na sio kufanya utafiti.

Alibainisha kuwa tuzo hiyo itatolewa kwa machapisho yote yanayokidhi vigezo kwa mwaka husika kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti na kwa mwaka huu wa fedha 2022/23, serikali imetenga Shilingi bilioni moja.

"Upatikanaji wa washindi wa tuzo hii utazingatia utaratibu na vigezo vilivyoainishwa katika mwongozo wa kitaifa ambao utazinduliwa leo na kuanza kutumika rasmi kushindanisha machapisho yaliyochapishwa ndani ya kipindi cha kuanzia Juni mosi, 2022 hadi Mei 31 mwaka huu. Tuzo hii itaanza kutolewa kwa machapisho katika fani za sayansi asilia na hisabati na tiba," alisema.

Alisema mchakato wa kupata washindi utasimamiwa na kamati ya tuzo ambayo itateuliwa na wizara kwa kuzingatia vigezo na uwiano ulioainishwa katika mwongozo wa tuzo.

"Tunaamini tuzo hii itaimarisha ubora, ushindani na morali kwa watafiti wa kitanzania na hatimaye kuongeza uzalishaji wa matokeo ya utafiti na ubunifu yenye tija kwa maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Prof. Mkenda alisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi na kuimarisha uwezo wa nchi katika kufanya utafiti na ubunifu unaolenga kuchagiza maendeleo ya uchumi wa viwanda na kuboresha maendeleo ya Watanzania.

# Zaidi watoto 170 wapata msaada bima ya afya

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

SHIRIKA la RHSC linalohudumia jamii inayoishi katika mazingira magumu hususani watu wenye ulemavu, limetoa msaada wa kadi za bima ya afya kwa watoto 172 katika Manispaa ya Iringa mkoani Iringa.

Watoto hao wenye ulemavu wanasoma Shule ya Msingi Ipogolo na Sabasaba na wanaotunzwa Kituo cha Nyumba Ali.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa Dk. Rita Kabati, alisema watoto wengi wenye ulemavu wanaishi kwenye mazingira magumu na kuwaomba wadau mbalimbali kujitokeza kuwasaidia.

"Tunajitahidi kutoa misaada mbalimbali kwa kushirikiana na wafadhili na watu wengine wenye mapenzi mema, lakini uhitaji ni mkubwa, hivyo tunawaomba Watanzania na wadau wengine wajitokeze kuwasaidia watoto wenye ulemavu," alisema Kabati.

Mbunge huyo ambaye ni balozi wa watu wenye ulemavu Tanzania, alilipia kadi za bima ya afya 150 kwa mwaka kwa watoto wenye ulemavu.

Kadhalika aliwapongeza wadau hao kwa kutoa msaada huo, huku akisisitiza watoto wenye ulemavu hawatakiwi kupata shida katika jamii.

Kuhusu vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watu wenye ulemavu, Kabati alisema unyanyasaji wa kijinsia mkoani Iringa unaongezeka.

Alitaka wahusika wote wa vitendo vya ukatili wabainike ili washughulikiwe ipasavyo kukomesha hali hiyo.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Jessica Mwalyoyo, alisema walianzisha 'mtoto bima day' baada yakubaini kuwa kuna watoto wengi wenye ulemavu wanaoshindwa kuhudhuria masomo siku nne kwa wiki kutokana na kuugua mara kwa mara na kukosa matibabu stahiki.

Mwalyoyo alisema kuwa wanufaika ni watoto 172 kutoka Shule ya Msingi Ipogolo kitengo maalumu, Shule ya Msingi Sabasaba kitengo maalum na kituo cha Nyumba Ali.

Mwenyekiti wa Shirika la Nyumba Ali Onlus, Zawadi Msigala, aliwashukuru wadau waliotoa msaada wa bima ya afya kwa watoto wenye ulemavu.

Alisema msaada huo umetoa mwanga kwa watu wenye ulemavu. Msigala mwenye ulemavu wa viungo anayetumia miguu yake kuandika, alisema kuwa watu wenye ulemavu wanapata shida za kiafya na kuiomba serikali kuweka mwongozo wa afya kwa watoto kupata matibabu bure kwenye vituo vya afya.

Alimwomba mbunge huyo kwenda kulipigia kelele suala hilo bungeni ili watoto wenye ulemavu wapate matibabu bila vikwazo.

Msigala ameandika kitabu chake kinachoitwa 'Ndoto Yangu' ambacho kinaelezea maisha yake akiwa shule ya msingi mwaka 2016.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 20/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HOSEA C. SALWA wa LUGALA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA STANLEY MLEWA SALWA NA KENETHI MLEWA SALWA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo **Tarehe 23 Mwezi 03 Mwaka 2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI - ICoT**

## TANGAZO LA KOZI YA MAOPARETA WA MITAMBO YA KAZI ZA UJENZI

**1. Utangulizi**

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology" (ICoT) ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yenye makao makuu katika Mkoa wa Morogoro kilipokuwa Chuo cha Ujenzi. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi ya Maopareta wa Mitambo ya Kazi za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi ya Maopareta wa Mitambo (Motor Grader Operators' Course). | **Wiki Kumi (10): kuanzia tarehe 17 Aprili hadi tarehe 23 June 2023** | **(ICoT – Morogoro)** |
| 2 | Kozi ya Maopareta wa TingaTinga (Bulldozer Operators' Course). | **Wiki Tano (5): kuanzia tarehe 22 May hadi tarehe 23 June 2023** | **(ICoT – Morogoro)** |
| 3 | Kozi ya Maopareta wa shindilia (Vibrating roller Operators' Course). | **Wiki Tano (5): kuanzia tarehe 22 May hadi tarehe 23 June 2023** | **(ICoT – Morogoro)** |

**2. Masomo Yatakayofundishwa**

Washiriki watajifunza moduli mbali mbali zinazohusu uendeshaji na utunzaji wa mitambo kama ifuatavyo: -

i. Kudumisha na kuweka usalama wa Mitambo na mahali pa kazi;
ii. Kufanya Ukaguzi na Matengenezo ya awali ya Mitambo;
iii. Uendeshaji na Utumiaji wa Mitambo katika kazi za Ujenzi na Matengenezo ya Barabara; na
iv. Kuweka kumbukumbu za Utunzaji wa Mitambo.

**3. Njia za Ufundishaji**

Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili kama ifuatavyo:

i. Kwa mafunzo ya mtambo wa Greda (Mortor grader): awamu ya kwanza itakuwa ni mafunzo ya nadharia (Darasani) yatakayofanyika kwa muda wa wiki nne (4) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site') yatakayofanyika kwa muda wa wiki sita (6); na
ii. Kwa mafunzo ya mtambo wa Tingatinga (Buldozer) na Shindilia (vibrating roller), mafunzo ya nadharia (Darasani) yatafanyika kwa muda wa wiki moja (1) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site') yatakayofanyika kwa muda wa wiki nne (4).

**4. Lugha ya Mafunzo**

Lugha itakayo tumika katika kozi ya Maopareta wa Mitambo itakuwa ni mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**5. Malengo ya Kozi**

Kozi hii inalenga kumpatia mshiriki uwezo na ujuzi wa kutumia mitambo katika kufanya kazi za Ujenzi na Matenegenzo ya Barabara. Mwisho wa Mafunzo inatarajiwa kuwa mshiriki atakuwa na uwezo wa: -

i. Kutumia Mitambo katika kufanya kazi ya ujenzi na matengenezo ya barabara;
ii. Kuhakiki usalama mahala pa kazi na utunzaji wa mtambo (Mitambo);
iii. Kufanya matengenezo ya awali pindi inapotokea hitilafu ndogo; na
iv. Kutunza kumbukumbu za mtambo.

**6. Sifa za Muombaji**

Mwombaji wa mafunzo haya anatakiwa kuwa nasifa zifuatazo:-

- Awe wa jinsia ya kike au kiume mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi;
- Awe na Kitambulisho cha NIDA au namba za Kitambulisho cha NIDA
- Awe na leseni halali ya udereva.

**7. Gharama za Mafunzo**

Gharama za kushiriki mafunzo ni kama ifuatavyo:-

i. Kwa mafunzo ya mtambo wa Greda (Motor grader), ada ya ushiriki ni shilingi za Tanzania Milioni Moja tuu (1,000,000);
ii. Kwa mafunzo ya mtambo wa Tinga tinga (Bulldozer) na mtambo wa Shindilia (vibrating roller) ada ya ushiriki ni shilingi za Tanzania laki saba (700,000).

Ada za ushiriki zitagharamia mafunzo na vifaa vya kuandikia tuu; mshiriki atajitegemea gharama za chakula na malazi.

Malipo ya ada ya ushiriki yafanyike wiki mbili kabla ya kuanza kozi kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mshiriki yeyote atakayehitaji kupata mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi wa Taasisi.

**8. Namna ya Kutuma Maombi**

Wale wote wenye sifa zilizoanishwa hapo juu na watakao hitaji kupata mafunzo haya, wanatakiwa kujiandikisha katika ofisi za Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ICoT Makao Makuu – Morogoro au Tawi la Mbeya (ICoT – Mbeya) kisha kufanya malipo kabla ya tarehe ya kuanza mafunzo. Unaweza kuwasiliana na msimamizi wa kozi (course guide) Hii Eng. MWAFULA kwa namba ya simu 0686220590 ili kupata ufafanuzi zaidi.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

| S.L.P 963, MOROGORO | | S.L.P 1957, MBEYA | |
|---|---|---|---|
| Simu : | 023- 2935229/023- 2935226 | Simu : | 025 295 7484/5; |
| : | 0686 220 590 / 0759 077 606 | : | 0764 775 354; 0769 317 404; 0765 251 509 |
| : | /0715 972 010 | Nukushi : | 025 295 7486 |
| Nukushi : | 023-2935227 | Barua pepe : | attimbeya@mow.go.tz |
| Barua pepe : | mwti@morogoro.net | | attimbeyafrica@gmail.com |
| Tovuti : | www.icot.ac.tz | Tovuti : | www.icot.ac.tz |

217340602



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere kwa niaba ya Mama Maria Nyerere kuibuka shujaa katika hafla ya Tuzo za Malkia wa Nguvu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ACT-Wazalendo yakunwa serikali kutenga bajeti mchakato Katiba mpya

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kimefurahishwa na tamko la Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, kwamba serikali imeshatenga fedha za bajeti kwa ajili ya mchakato wa Katiba mpya na marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Uchaguzi.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wake Bara, Dorothy Semu wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Katiba na Sheria Machi 24, mwaka huu, Dk. Ndumbaro alisema mchakato wa Katiba mpya pamoja na marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa na uchaguzi unatarajiwa kuanza kufanyiwa kazi baada ya kupitishwa kwa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2023/24.

Semu alisema: "Tumefurahishwa na tamko la Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumaro, kwamba sasa serikali imetenga fedha za bajeti kwa ajili ya mageuzi haya ya kisiasa. Hii ni hatua kubwa na itawezesha angalau kupata sheria mpya ya vyama mwaka huu. ACT-Wazalendo itaendelea kufuatilia kwa karibu mchakato huu."

Pia, aliiomba serikali kuharakisha hatua za utekelezaji wa masuala hayo kwa kutoa ratiba kama ilivyo kwenye mapendekezo ya kikosi kazi hatua kwa hatua ili itakapofika Novemba mwaka huu kuwe kumepatikana sheria hiyo.

Alisema wanaamini endapo serikali itafanya hivyo, wanatarajia hata marekebisho ya mchakato wa Katiba mpya yatafanyika kwa uharaka.

Semu alitoa wito kwa asasi za kiraia na vyama vya kijamii kutoa shinikizo kwa serikali kuchukua hatua stahiki ili kuleta mageuzi ya siasa nchini.

Alisema: "Kupitia majukwaa ya kisiasa kama vile Baraza la Vyama vya Siasa na Kituo cha Demokrasia nchini waanze mijadala katika ngazi ya mikoa na wilaya kuhusu mapendekezo ya kisheria ili kuhakikisha kwamba uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa unakuwa huru na haki."

"Na tunavisihi vyama vyote vya siasa kuwa upande mmoja ili kufanikisha mageuzi haya na kuepuka kuwa na njia zisizo rasmi ambazo zaweza kuchelewesha mchakato wa mageuzi muhimu."

# Vijana 155,000 wapewa mafunzo ujuzi, ufundi

**Na Restusta James**

VIJANA 155,000 wamepewa mafunzo ya ujuzi wa ufundi mbalimbali kupitia ufadhili wa serikali katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Taarifa ya Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi (VETA), iliyotolewa mwishoni mwa wiki ilieleza kuwa mafunzo hayo yalifadhiliwa na serikali kupitia tozo ya ujuzi na kwa ushirikiano na wadau.

Ilieleza kuwa vijana 140,124 kati yao walipata mafunzo kwenye vyuo vya VETA kupitia tozo ya kuendeleza ujuzi kupitia Mpango wa Uanagenzi ulioratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) na vijana 10,456 walifadhiliwa kupata mafunzo katika vyuo vya VETA.

Katika taarifa hiyo, VETA ilieleza kuwa vijana wengine 420 walinufaika na mafunzo ya teknolojia ya kutengeneza vihenge vya chuma kwa ajili ya kuhifadhia mazao ili kutatua tatizo la usalama wa chakula hususani udhibiti wa sumukuvu.

Ilieleza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) na VETA, ilifadhili wanafunzi 4,000 kupitia mradi wa kikanda wa ajira na ujuzi kwa maendeleo ya Afrika ambao wanaendelea na mafunzo kwenye vyuo mbalimbali vya VETA.

"Jitihada mbalimbali za kuimarisha ubora wa mafunzo zimefanyika kupitia uhuishaji wa mitaala ya kufundishia pamoja na ununuzi wa mitambo, zana na vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia. Jumla ya mitaala 48 imehuishwa ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira na mwenendo wa nchi kiuchumi," ilieleza taarifa hiyo ya VETA. Inaeleza kuwa mapendekezo ya sera mpya ya elimu yametoa kipaumbele kikubwa kwenye elimu ya ufundi stadi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika kipindi cha miaka miwili cha serikali ya Rais Samia, vyuo 33 vya VETA vimejengwa na kuwekewa samani na kwamba lengo la uboreshaji wa vyuo vya ufundi ni kutoa ujuzi stahiki ili wahitimu waweze kujiajiri na kuajiriwa.

Kadhalika, serikali inaendelea kujenga vyuo vya ufundi katika wilaya zote nchini kuanzia mwaka huu wa fedha.

# TAA kuboresha viwanja vya ndege kuvutia wawekezaji

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mussa Mbura, amesema wataendelea kuboresha viwanja vya ndege nchini ili watumiaji wapate huduma bora zinazokidhi na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mbura aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mgahawa wa kisasa wa Sky View uliofunguliwa ndani ya jengo la abiria wanaosafiri kwenda nje ya nchi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Terminal III wa Julius Nyerere (JNIA) uliogharimu Dola za Kimarekani 500,000.

Alisema Tanzania ina viwanja vya ndege 58 huku akiwataka wawekezaji kuwekeza katika utoaji wa huduma katika viwanja hivyo kikiwamo cha JNIA na kipya kilichojengwa Arusha.

Mbali na viwanja hivyo wawekezaji wanakaribishwa katika viwanja vya Mbeya, Katavi, Mwanza na kiwanja cha Kimataifa cha Msalato, mkoani Dodoma ambacho ujenzi wake bado unaendelea.

Aidha, alisema wanafanya juhudi mbalimbali za kuhakikisha JNIA inakuwa na huduma bora na zenye viwango ambazo wateja wanastahili kupatiwa wanapokuwa viwanja vya ndege.

Alisema wawekezaji wa Sky View ambao ni wazalendo walionyesha nia ya kuwekeza kuhakikisha wanatoa huduma hiyo kwa wateja.

Mbura alisema huduma hiyo ni ya kwanza kutolewa nchini, wanawashukuru na wanaamini kutakuwa na ongezeko la wateja katika mgahawa huo.

"Sisi kama mamlaka tumekuwa tukiwapa ushirikiano tangu walivyoanza hadi sasa. Kufunguliwa kwa huduma hiyo katika uwanja wetu kunaendana na agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha wanaongeza uwekezaji," alisema Mbura.

Alisema yaliyofanyika ni juhudi za Rais Samia za kutaka kuwapata wawekezaji zaidi katika maeneo hayo na tayari wameanza kwa vitendo.

Aidha, alisema anampongeza Rais Samia kuwapo kwa mazingra mazuri ya uwekezaji nchini na kuwakaribisha wawekezaji katika viwanja vyao vya ndege.

Alisema faida wanazozipata ni mapato na moja ya mikakati yao ni kuongeza mapato na kuwataka wawekezaji hao kuwa waaminifu ili nchi inufaike kukuza uchumi wake.

Naye Mkurugenzi wa SKY View, Brigedia Jenerali mstaafu Michael Luwongo, alisema wanaishukuru TAA kuiamini kampuni ya kitanzania kufanya uwekezaji huo.

Alisema Rais Samia amefanya maboresho mazuri ya uwekezaji na hata wakihitaji msaada serikali inatoa ushirikiano ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

"Tunamshukuru Rais Samia kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ambayo hivi leo tunayashuhudia na kuyafurahia, tutaendelea kushirikiana na serikali na hata tutakapokosea tupo tayari kukosolewa kwani hii ni sehemu ya kutujenga na huduma zetu kuwa bora zaidi," alisema.

Pia alibainisha kuwa uwekezaji huo umegharimu Dola za Kimarekani 500,000 na wamewekeza katika miradi mingine ikiwamo miwili iliyopo JNIA.

# Wadau watoa mbinu kuboresha kilimo alizeti

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa alizeti nchini wameishauri serikali na watafiti kuzalisha mbegu bora ili zipatikane kwa bei nafuu tofauti na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na kuuzwa bei ya juu.

Vilevile, wameiomba serikali kuzuia uingizwaji wa mafuta yatokanayo na zao hilo kutoka nje nchi kwa kuwa unachangia kushuka kwa bei kwa yanayozalishwa nchini na kuua soko la ndani hali inayokatisha tamaa wakulima.

Ushauri huo umekuja ikiwa ni wiki moja tangu Rais Samia Suluhu Hassan kuwataka Watanzania kuendelea kuzalisha chakula kwa wingi ili waendelee kuilisha dunia, wakati akizindua mpango wa mashamba makubwa chini ya mradi wa mpango wa kesho iliyobora (BBT) mkoani Dodoma.

Mkulima wa alizeti kutoka Singida, Dk. Henry Mbando, alisema serikali kwa kushirikiana na wataalamu wa utafiti wafanye utafiti ili ipatikane mbegu bora inayozalisha kwa wingi itakayouzwa kwa bei nafuu kwa kuwa iliyopo sasa inatoka nje ya nchi na inapatikana kwa bei ya juu.

Alisema serikali iongeze upatikanaji wa mbolea ya ruzuku kwa kuwa iliyopo sasa ni chache na hivyo wakulima wengi hasa wenye mashamba makubwa hawaipati hali inayowalazimu kununua ya bei kubwa.

"Mbegu iliyo bora aina ya hysun kwa sasa inapatikana kwa Sh. 48,000 kwa kilo na heka moja inaingia kilo mbili, hapo heka moja unatumia Sh. 90,000 kwa sisi wenye heka 400 unaona namna tunavyotumia gharama kubwa, lakini tukiwa na mbegu ya kutosha inayozalishwa hapa nchini gharama zitashuka," alisema.

Joseph Kisiriri, alisema kitendo cha serikali kuruhusu mafuta ya kula kuingizwa kutoka nje ya nchi kinasababisha yanayozalishwa ndani kushuka bei na wakulima kuumia kwa kuwa wanatumia gharama kubwa ya uzalishaji.

"Haya mafuta yanavyoingizwa nchini na kuuzwa bei ya chini, sisi wazawa ya kwetu tukauze wapi? Dumu la mafuta la lita 20 kwa sasa linauzwa Sh. 60,000 kutoka Sh. 100,000, hii inatuvunja nguvu wakulima inafika mahali tunaona tusilime kwa sababu tunapata hasara, serikali iliangalie hili," alisema.

James Sabore, anayemiliki heka 600 za shamba la alizeti alisema serikali pia iwakumbuke wakulima wakubwa kwenye mikopo ya pembejeo na zana za kilimo kama matrekta na dawa za kuulia wadudu ili kurahisisha shughuli za uzalishaji.

"Lakini kuna suala la mabadiliko ya tabianchi ambalo linaleta changamoto katika uzalishaji wetu, serikali inapaswa itusaidie tupate miundombinu na vifaa vya mikopo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kwa sababu wakati mwingine Singida inakuwa kame na mvua hazitabiriki, hii ni shida kubwa kwetu," alisema.

Aliiomba serikali iwatafutie soko la uhakika kwa kuwa hiyo imekuwa changamoto ya muda mrefu inayokatisha tamaa wakulima na kufikia hatua ya kupunguza uzalishaji na wengine kuacha shughuli hiyo jambo linalopunguza kasi ya uzalishaji.

Mwenyekiti wa Chama cha Wasindika Alizeti Tanzania, Ringo Irigo, alisema uchache wa viwanda vya ndani vya kuzalisha mbegu bora unachangia mbegu hizo kuuzwa kwa bei ya juu.

"Tatizo ni kwamba kiwanda kinachotengeneza mbegu hizo kipo kimoja ambacho huuza kilo moja Sh. 15,000 kwa hiyo soko halijitoshelezi, naishauri serikali pamoja na watafiti kama TARI wabuni mbegu za kutosha za aina hii ili wakulima wanunue kwa wingi uzalishaji uwe mkubwa," alisema Ringo.

Alisema anaishukuru serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuanzisha mashamba makubwa ya kilimo cha mazao ya kimkakati ikiwamo alizeti kwa kuwa yatasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao hayo na kushauri isijikite kwa vijana pekee.




Wadau wa sekta ya muziki wakishiriki mjadala kuhusu namna ya kuwawezesha wasanii wa kike kupambana na changamoto wanazokutana nazo. Mjadala huo ulifanyika mwishoni mwa wiki ulioandaliwa na Mdundo kwa udhamini wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL). Kutoka kushoto ni msanii Mwasiti, Ofisa Mwandamizi COSOTA, Naomi Mungule, Mtangazaji wa Radio, Mamy Baby, Mkuu wa Uvumbuzi SBL, Bertha Vedastus na Elias Maeda, mwanzilishi wa Medea Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabaharia watunukiwa vyeti kutambuliwa kimataifa

**Na Restuta James**

MABAHARIA 35 kutoka Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, wametunukiwa vyeti vyenye hadhi ya kimataifa na Shirika la Bahari Duniani (IMO).

Mabaharia hao ambao wengi ni wakufunzi kutoka DMI walitunukiwa vyeti hivyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, baada ya kuhitimu mafunzo yaliyotolewa na wataalamu kutoka IMO.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TASAC wakati wa kufunga mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Huduma za shirika hilo, Rajab Mabamba, alisema mabaharia waliotunukiwa vyeti wamepata mafunzo ya mkataba wa kimataifa wa viwango vya mafunzo na utoaji wa vyeti na ufanyaji kazi wa mabaharia ambao Tanzania imeuridhia.

"Mafunzo yote yanayotolewa kwenye fani ya ubaharia yanasimamiwa na mkataba huu. Kwa kushirikiana na IMO kwa kugundua kwamba kulikuwa na upungufu, tumeona ni vizuri tukawa na wataalamu ambao wanaweza kufanyakazi ndani lakini pia kwenye nchi nyingine," alisema.

Alisema mabaharia waliopata mafunzo hayo watapaswa kurithisha utaalamu walioupata kwa wakufunzi wenzao pamoja na wanafunzi ili Tanzania iwe na mabaharia wengi wenye sifa za kimataifa.

Mabamba alitoa wito kwa vijana kuingia kwenye fani ya ubaharia kwani kuna fursa nyingi akitaja mojawapo ni kuelekea uchumi wa bluu.

"Ubaharia ni kazi ambayo ajira na fursa zake ziko kimataifa na kuna upungufu wa wataalamu katika fani hii," alisema Mabamba.

Naye Mkufunzi kutoka DMI, Kapteni Haruna Ally, alisema mafunzo hayo yanatoa nafasi ya kuwatambulisha mabaharia wanaotoka DMI kutambuliwa na waajiri nchi yoyote.

Alisema mafunzo hayo yamewapa mbinu za kufundisha kwa namna ambayo haimkaririshi mwanafunzi bali kumpa ujuzi utakaomwezesha baharia wa Tanzania kushindana kwenye soko la ajira.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa siku tano na kwa utaratibu wa IMO, shirika hilo litakuwa linafanya ukaguzi kila baada ya miaka mitano ili kuona kama chuo kinatoa mafunzo kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

# Vijiji 3 kunufaika mradi wa maji wa bil. 1/-

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI zaidi ya 8,558 wa vijiji vya Kichiwa, Tagamenda na Maduma Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, mkoani Njombe wanatarajia kunufaika na mradi wa maji wenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni moja unaotekelezwa na mkandarasi Nyagawa Trades.

Akizungumza katika utiaji saini mkataba wa utekelezaji wake, Mhandisi Elikalia Malissa, alisema vijiji hivyo ni miongoni mwa visivyokuwa na maji.

"Katika mradi huu kuna kazi ambazo zitakwenda kufanyika ambazo ni ujenzi wa chanzo, ulazaji wa bomba kuu kilometa 32, ujenzi wa tangi lenye ujazo wa lita 150,000, vituo 15 pamoja na nyumba ya michango," alisema Malissa.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alimtaka mkandarasi kumaliza kazi hiyo kwa wakati na kwa ubora, "kwa upande wa usimamizi ndugu zangu wenyeviti wa vijiji, watendaji na viongozi wote chama kuanzia ngazi ya kata na matawi nyinyi mpo kule haiwezekani mradi ukasuasua halafu nyinyi mpo, tunaomba sana mtupe taarifa kwenye yale mnayoweza kuchukua hatua mchukue hatua," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Edwin Swalle, aliwaomba wakala wa maji vijijini RUWASA mradi huo ufanyike kwa nguvu inayotakiwa ili kuondoa hofu kwa wananchi ya ucheleweshwaji wa miradi ya maji iliyotokea huko nyuma.

"Mkandarasi aliyepewa kazi naamini anauwezo mzuri ana uzoefu, tumsaidie mradi huu ukamilike mapema ili wananchi hawa wakishamshukuru Rais kwa kazi hii ambayo leo wanaiona pia washuhudie wanapokunywa maji," alisema Swalle.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Njombe, Justin Nusulupila, alisema ili miradi ya maji iweze kudumu kwa muda mrefu ni vyema wananchi wakaelimishwa waache kulima kwenye vyanzo vya maji na kupanda miti rafiki wa mazingira.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars msibweteke, jipangeni Uganda idondoshe zote sita

**BAADA** ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini nchini Misri dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda, Taifa Stars kesho, Jumanne itawakaribisha Waganda hao katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwenye mechi ya marudiano ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023.

Taifa Stars ambayo ipo Kundi F, linaloongozwa na Algeria iliyopo kileleni baada ya kujikusanyia pointi tisa hadi sasa, inashika nafasi ya pili ikiwa na alama nne ikifuatiwa na Niger yenye pointi mbili na Uganda ikiburuza mkia baada ya kuambulia alama moja tu katika mechi zake tatu.

Ni wazi Algeria ina nafasi kubwa ya kuongoza kundi hilo, hivyo timu tatu Tanzania, Niger na Uganda zina kibarua kigumu cha kuwania nafasi moja ya kuungana na Waalgeria hao kufuzu fainali hizo za Afcon zitakazofanyika nchini Ivory Coast mwakani.

Kwa namna msimamo wa kundi hilo ulivyo, tunaamini kama Taifa Stars itautumia vema uwanja wake wa nyumbani katika michezo miwili itakayocheza Benjamini Mkapa, dhidi ya Uganga na baadaye Niger, inaweza kufuzu kwa mara ya tatu katika historia yake kwenye fainali hizo zenye utajiri mkubwa barani Afrika.

Kinachotakiwa ni wachezaji wa Taifa Stars kutobweteka baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Uganda katika mchezo uliopita, kwani hii ni mechi nyingine ambayo wapinzani wao wataingia na mbinu tofauti baada ya kujua uchezaji wao, lakini pia Waganda hao wanatambua kabisa kudondosha tena alama tatu dhidi ya Tanzania kutazidi kuwaweka katika nafasi finyu ya kufuzu fainali hizo.

Hivyo ni wakati sasa kwa Taifa Stars, kusahau matokeo yaliyopita na kuingia uwanjani na mbinu tofauti kabisa kama vile wanakwenda kukutana na timu ambayo hawajawahi kucheza nayo, lakini kila mchezaji atakayepewa dhamana ya kuvaa jezi ya taifa kutambua anawakilisha zaidi ya Watanzania milioni 61.

Tunatambua haitakuwa mechi rahisi hasa kutokana na rekodi nzuri Uganda iliyo nayo dhidi ya Tanzania timu hizo zinapokutana katika michuano mbalimbali, jambo ambalo kila mchezaji anapaswa kuvuja jasho haswa.

Ikumbukwe hii itakuwa ni mara ya 61 kwa Taifa Stars kukutana dhidi ya Uganda (The Cranes), huku Waganda hao wakishinda mara 32, wakipoteza mara 13 tu na sare 15, rekodi ambazo zinaendelea kuibeba zaidi pamoja na kupoteza mchezo uliopita.


Tunachotaka kukiona ni wachezaji wa Taifa Stars kusahau ushindi huo na rekodi mbaya dhidi ya Waganda hao na kisha kushuka dimbani kwa kupambana mwanzo mwisho kwa lengo moja tu la kupata matokeo katika mchezo huo muhimu kwao kabla ya ratiba ijayo kuikaribisha Niger uwanjani hapo.

Tahadhari nyingine tunayoitoa kwa Stars ni kutocheza na jukwaa hasa ikizingatiwa watakuwa wakipata sapoti kubwa kutoka kwa mchezaji wao wa 12 uwanjani hapo, ambao ni mashabiki watakaofurika Benjamin Mkapa kuishangilia.

Hatutarajii kuona mbwembwe nyingi zisizo na maana kwa wachezaji kutaka kushangiliwa na mashabiki, badala yake tunataka kuona mpira ukitembea kwa kasi zaidi kuelekea lango la mpinzani kwa kuwa kinachotakiwa ni matokeo kwanza kabla ya mambo yote.

Lakini pia ni wakati wa mashabiki kununua tiketi kwa wingi na kujitokeza uwanjani kuiunga mkono Stars ili iweze kupata matokeo na hatimaye kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu fainali hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wageni wamepandisha kiwango cha Stars

**SIMON** Msuva, mfungaji pekee wa bao la Taifa Stars Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Suez Canal, Ismailia nchini Misri dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda, The Cranes, amekiri kuwa kiwango cha soka Tanzania kwa ngazi ya klabu na timu ya taifa kwa sasa kinaonekana kupanda kwa kasi.

Winga huyo anayekipiga Klabu ya Al-Qadsiah ya Saudi Arabia, amesema Tanzania kwa sasa iko juu kisoka katika ngazi zote, baada ya timu za Simba na Yanga kufanikiwa kutinga hatua za robo fainali ya michuano ya kimataifa, na Stars kufanya vema kwenye mechi hiyo ya Ijumaa ya kusaka tiketi ya kufuzu Mataifa ya Afrika kwa kuitwanga Uganda bao 1-0.

Tanzania ina nafasi kubwa ya kwenda Afcon kama itachanga vema karata zake kwa kushinda mechi ya kesho dhidi ya Uganda, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na nyingine dhidi ya Niger ambayo itachezwa hapa nchini.

Kiwango kilichooneshwa kwenye mechi iliyopita kiliwakuna mashabiki wengi na kwa kiasi kikubwa Watanzania wengi walifurahi.

Wachezaji wengi walionesha viwango vya hali ya juu na kuwafunika Waganda licha ya kujitutumua.

Lakini si wengi wanaojiuliza ni kwa nini wachezaji Stars wameonesha kiwango kikubwa vile? Ni ukweli ambao baadhi ya watu utakuwa mchungu kwao kwa sababu hawataki kulisikia hili. Ni kuwapo kwa wachezaji wengi wa kigeni wanaocheza soka la kulipwa nchini.

Uwapo wa wachezaji wengi kutoka nje ya nchi wanaocheza soka la kulipwa hapa nchini, umewafanya wachezaji wa Kitanzania kutohofia na wala kutokuwa na wasiwasi kucheza na wachezaji kutoka mataifa mengine. Kwa sababu baadhi yao wanacheza nao hapa nchini.

Huko nyuma wakati zaidi ya asilimia 90 Ligi Kuu Tanzania ilikuwa na wachezaji wa Kibongo, wachezaji wetu walikuwa wanapata tabu sana kwa sababu utaona wanakuwa hata na wasiwasi wanapotuliza mpira. Watauondoa haraka na kupiga mbele kwa sababu hawataki kukosea.

Mfano ukiangalia mechi iliyopita pale kati ya Waganda walikuwa na Khalid Aucho anayecheza Klabu ya Yanga. Pamoja na kwamba alikuwa kwenye kiwango kizuri, lakini viungo wa Stars waliweza kumdhibiti mara kwa mara kwa sababu wanamfahamu, wanacheza na kukutana naye kwenye ligi, na wengine wanakuwa naye mazoezini.

Kulikuwa na Emmanuel Okwi ambaye alishawahi kuichezea Simba na Yanga, mabeki wa Stars kwa sababu wanamfahamu ni winga mjanja na mkorofi, walifanikiwa kumdhibiti kwa sababu wanamfahamu.

Wengi hawaoni faida ya kuwa na wachezaji wa kigeni wanaocheza soka nchini, badala yake wanaona wanawafanya wachezaji wa Kitanzania wasipate nafasi kwenye klabu zao. Wengine wanaomba hata wachezaji wa kigeni kwenye Ligi Kuu wapunguzwe, bila kujua kuwa si lazima wachezaji wa Stars waitwe kutoka Simba, Yanga au hata ndani ya nchi.

Tukumbuke Senegal imeita wachezaji wote kutoka Ulaya, kasoro mmoja tu, naye hatoki ndani ya nchi yao, bali anacheza bara la Afrika, naye ni Pape Sakho tu kutoka Simba.

Leo hii Stars ikicheza dhidi ya Senegel, Congo DR, Mali, Zambia, Zimbabwe, wachezaji wake hawatokuwa na kitete kwa sababu wanakutana na wachezaji ambao wanawafahamu na wanacheza nao kwenye ligi kina Prince Dube, Clatous Chama, Kennedy Musonda, Djigui Diarra, Henock Inonga, Fiston Mayele na wengineo.

Ni sawa na kwenda sehemu ambayo ni ngeni, lakini kwa bahati nzuri ukikutana na mtu ambaye unamfahamu ama ulishawahi kukutana naye huko nyuma na ni mwenyeji wa hapo, unakuwa si mgeni tena na unachangamka kama vile wewe ndiye mwenyeji.

Chochote kitakachofanyika ili kupunguza wachezaji wa kigeni kwenye klabu zetu, si kwamba zitazifanya klabu za Simba na Yanga kutofanya vema tena kwenye michuano ya kimataifa kwa sababu wanaozibeba kwa asilimia kubwa ni wageni, lakini hata timu ya taifa itashuka kiwango.

Kwa sababu wachezaji wetu watakuwa hawana kazi ya kuvuta soksi na kugombania namba na wageni kwenye klabu zao kitu ambacho kinawafanya wapandishe viwango na kuchaguliwa Stars, lakini pia watakuwa na hofu na wachezaji wapya wanaokutana nao kwenye vikosi vya nchi nyingine.

Upinzani wa namba wanaoupata kwenye klabu zao, pamoja na kukutana na baadhi ya wachezaji wanaocheza nao kwenye ligi, unawafanya wajiamini na kucheza bila presha, hivyo ukiongeza na wachezaji kama kina Msuva na Mbwana Samatta, kiwango cha wachezaji Stars kimekuwa juu na hali ikizidi kuendelea itazidi kushangaza wengi.

# Serikali kuendelea kudhibiti taka za vifaa vya mawasiliano kielektroniki

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema serikali itaendelea kuzingatia hatua endelevu za kutekeleza wajibu wa kudhibiti taka za vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki kwa kuwataka watengenezaji na waagizaji wa vifaa hivyo kutimiza wajibu wao.

Alisema hatua hiyo inalenga kupunguza athari za kimazingira zinazotokana na ongezeko la taka za kielektroniki hasa kutoka vifaa vya mawasiliano kama simu za mkononi na kompyuta.

Waziri Nape alikuwa akifungua warsha ya Kudhibiti Taka za Kielektroniki iliyofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam ikiwashirikisha wadau wa mawasiliano kutoka nchi wanachama wa Taasisi za Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO), Afrika na Ulaya.

Warsha hiyo iliyoandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilikuwa na kaulimbiu: "Kutoka kufahamu hadi kuchukua hatua: Kuchukua hatua endelevu za kudhibiti taka za kielektroniki kama kipaumbele kuelekea kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya mwaka 2030."

Uwapo wa Waziri Nape katika ufunguzi wa warsha ni ishara ya wazi ya dhamira ya Serikali ya Tanzania kufanya kazi kwa karibu na washirika wa udhibiti wa taka za kielektroniki ili kuhakikisha njia endelevu na zenye ufanisi za kudhibiti taka za kielektroniki zinapatikana na kufikiwa ili kupunguza hatari za kimazingira na afya zinazohusiana na taka za aina hiyo.

"Taka za kieletroniki ni moja ya taka zinazokua kwa kasi zaidi ulimwenguni ambazo ni sumu na haziozi, ongezeko la kasi la aina hii ya taka ni matokeo ya kuongezeka kwa matumizi ya vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki pamoja na ukuaji wa mabadiliko katika mifumo ya teknolojia za kidijitali nchini. Tanzania iko katika hatua za awali za kuhakikisha kunakuwapo wajibu kwa wazalishaji na waagiza wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki," alisisitiza Waziri Nape.

Baadhi ya mapendekezo yaliyofikiwa kwenye mkutano huo ni pamoja na kuendesha kampeni zaidi za uelewa, kuimarisha ushirikiano na wadau wote wa usimamizi wa taka za kielektroniki na kusaidia uboreshwaji au uundaji wa mtaala wa taasisi za elimu ya juu utakaosaidia udhibiti wa taka za kielektroniki.

Washiriki pia waliomba serikali kutenga fedha kwa miradi ya usimamizi wa taka za kielektroniki na kuunda mfumo wa kitakwimu utakaowezesha kubaini na kuunganisha nguvu za wadau katika kudhibiti taka hizo. Kulikuwa pia na mapendekezo ya kuendelea kutekeleza Mkakati wa Pili wa Usimamizi wa Taka za Kielektroniki wa Kikanda sambamba na kuboresha zaidi juhudi za pamoja za kikanda ili kudhibiti taka za kielektroniki.

Mapendekezo mengine muhimu yalikuwa kutunga sheria maalum za usimamizi wa taka za kielektroniki ili kuboresha usimamizi wa taka za vifaa vya elektroniki katika Kanda ya Afrika Mashariki.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema mamlaka hiyo imekuwa ikifanya utafiti mbalimbali kwa lengo la kutafuta njia za kusimamia taka za kielektroniki.

Alisisitiza kuwa TCRA imeweka mikakati ya kuhakikisha kuwa taka za kielektroniki zinadhibitiwa kwa kutoa elimu kwa watumiaji juu ya jinsi ya kuviondoa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki baada ya muda wake wa matumizi kufika tamati.

"TCRA tayari imeanza kufanyia kazi utekelezaji wa kuweka wajibu wa wazalishaji na waagizaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki kupitia mfumo wa uwajibikaji wa wazalishaji, ambapo watahitajika kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya mawasiliano vya kielektroniki vinapimwa na kuidhinishwa ili kuzuia uagizaji wa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki ambavyo vimemaliza muda wake," alisisitiza Jabiri.

"Hii imekuwa warsha yenye mafanikio zaidi nadhani Tanzania imewapa changamoto waandaaji wengine wa semina kama hii," alibainisha Katibu Mtendaji wa EACO Dk. Ally Yahaya Simba.



Mbunge wa Mchinga mkoani Lindi, Salma Kikwete (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Coca Cola, Unguu Sulai (wa tatu kulia), Meneja Masoko wa Oryx Gas Tanzania, Peter Ndomba (wa tatu kushoto), Meneja Uhusiano wa Coca Cola, Salum Nasoro (wa pili kushoto) wakiwa na mmoja wa wanawake wenye ulemavu (kushoto) wakimkabidhi jiko la Oryx lililotolewa bure kwa mamalishe hao kupitia programu ya Mwanamke Shujaa inayoratibiwa na kuandaliwa na Coca Cola. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye dalili TB watakiwa kuwahi vituo vya afya

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WANANCHI katika Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi wametakiwa kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wanapoona dalili za ugonjwa wa kifua kikuu ili kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Gilbert Bayaga, wakati wa maadhimisho ya ugonjwa huo duniani.

Bayaga alisema moja ya sababu zinazosababisha ugonjwa wa kifua kikuu ni lishe duni hali inayosababisha kushuka kwa kinga ya mwili na kupata ugonjwa huo kwa urahisi.

Alisema kwa Manispaa ya Mpanda wagonjwa wa kifua kikuu wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka, tangu mwaka 2019 hadi 2022 kumekuwa na wagonjwa 1,200.

Bayaga alisema kuna ongezeko la wagonjwa kutoka wagonjwa 253 kwa mwaka 2019 hadi wagonjwa 431 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 41.

Mratibu wa ugonjwa wa kifua kikuu na ukoma katika Manispaa ya Mpanda, Bruno Cornely, alisema mpaka sasa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ina vituo vya kutolea huduma za afya 30, kati ya hivyo, vinavyotoa huduma ya kupima makohozi ni sita, vya serikali ni vinne na binafsi ni viwili.

Alisema uhamasishaji na uchunguzi wa kifua kikuu ngazi ya vituo unaendelea ikiwa ni pamoja na kufanya uhamasishaji wa usafirishaji wa sampuli za makohozi kwenda kwenye vituo vinavyopima ugonjwa huo.

Pia alisema wamekumbana na matatizo mbalimbali ikiwamo ufinyu wa bajeti ngazi ya halmashauri kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo, vifo vitokanavyo na kifua kikuu kuendelea kurekodiwa, mwaka 2021 vilikuwa 33 sawa na asilimia 7.9.

Alisema vifo hivyo vilisababishwa na kuchelewa kuanza matibabu kwa baadhi ya wagonjwa.

Hata hivyo, alisema halmashauri imejipanga kwa kuweka mikakati mbalimbali ili kufika malengo kwa mwaka huu ikiwa ni pamoja na kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii kufuatilia na kutembelea familia zilizo na wagonjwa na kufanya uchunguzi ngazi ya familia ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya afya ya uzazi.

Alisema watashirikisha wamiliki na wauza maduka ya dawa katika kuibua wagonjwa wa kifua kikuu masuala ya ugonjwa huo kuyafanya kuwa ajenda ya kudumu kwenye vikao mbalimbali vya halmashauri na ngazi ya jamii.

Baadhi ya wananchi akiwamo, John Mtaturu, waliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya hasa kwa wagonjwa wa kifua kikuu ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya unyanyapaa kwa wagonjwa ikilinganishwa na awali wagonjwa walikuwa wakitengwa.

# Wananchi wapewa hadhari kesi ardhi zisizo za lazima

**Na Hassan Mabuye,** KATAVI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amewataka wananchi kuepuka kesi na mashtaka yasiyo ya lazima yanayowasilishwa katika mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya.

Aliyasema hayo juzi mkoani Katavi wakati wa uzinduzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mlele.

Pinda alitoa angalizo hilo alipokutana na mkazi wa Mpanda, Peter Lukas, mwenye kesi na mwenzake ambayo inaweza kutatuliwa kwa kukubaliana bila kuifungua katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

"Kesi nyingine ni ndogo sana na zinahitaji tu kauli za watu wawili, lakini mtu anazunguka nayo hiyo kesi ya ekari moja miaka 10 mpaka mashtaka yanaibuka, kumbe kama mngekuwa na uwezo wa kukubaliana mkakaa pamoja mngeweza kuelewana bila hata kufika katika mabaraza ya ardhi ya ardhi na nyumba ya wilaya," alisema Pinda.

Alisema kuwa wananchi wanatakiwa kuepuka mashtaka ya mara kwa mara kwa sababu kuendesha kesi ni gharama hasa katika kutafuta ushahidi, mawakili na hata katika kuisimamia mpaka kupatikana hukumu.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri Pinda alikutana na watumishi wa sekta ya ardhi, mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya pamoja na kukutana na watumishi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na amepokea taarifa za utendaji kazi pamoja na kutoa maelekezo.

Pia alikagua Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mpanda na kukagua ujenzi wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) za Wilaya ya Mlele mkoani Katavi.



Makamu Mwenyekiti Bara wa Chama cha ACT- Wazalendo, Dorothy Semu (kulia), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu mrejesho wa mikutano ya hadhara kwa awamu ya kwanza katika mikoa kumi ya Tanzania na Zanzibar. Katikati ni Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu na Waziri Kivuli Sekta ya Uwekezaji, Mashirika ya Umma na Hifadhi ya Jamii, Mwanaisha Mndeme. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# RPC ahadharisha biashara usafirishaji binadamu

**Na Baraka Jamali,** MTWARA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Nicodemus Katembo, ameitaka jamii kuwa makini na usafirishaji haramu wa binadamu na kuepuka udanganyifu kwa familia za kusini mwa Tanzania baada ya baadhi ya vijana wao kuchukuliwa kwa ajili ya kwenda kufanyakazi za ndani na badala yake kuuzwa nje ya nchi.

Akifungua mafunzo ya siku nne ya namna ya kudhibiti wimbi la biashara haramu ya usafirishaji binadamu yaliyoandaliwa na Shirika la Tanzania Relief Initiatives (TRI), kwa maofisa ustawi wa jamii, alisema vijana wengi wanachukuliwa na kupelekwa nje ya nchi kuuzwa.

"Mkoa wa Mtwara ni miongoni mwa mikoa ambayo vijana wanachukuliwa kwa kudanganywa wanakwenda kufanya kazi za ndani Zanzibar, lakini wengine wanasafirishwa nje ya nchi kwenda kuuzwa kwenye madanguro, yatupasa sisi sote tushirikiane kudhibiti vitendo hivi vya ovyo."

"Vijana wengine wanasafirishwa kwenda kuungwa kwenye makundi ya wahalifu Msumbiji na Congo na kuanzia kipindi cha Aprili 2022 mpaka sasa hapa nchini vijana wapatao 151 wamechukuliwa katika biashara haramu ya binadamu, kesi 13 zinaendelea mahakamani na wafanyabiashara sita wanatumikia vifungo gerezani," alisema.

Awali, akieleza dhamira ya mafunzo hayo, Mkurugenzi wa TRI, Edwin Mugambila, alisema ni kutoa elimu ya kutosha katika makundi muhimu ya kupambana na biashara hiyo haramu ya usafirishaji binadamu hususani maeneo ambayo ni rahisi kuwasafirisha.

Elimu hiyo imetolewa kwa mahakimu, ustawi wa jamii, polisi Magereza, Uhamiaji na wanahabari, ili waweze kuisaidia jamii kukemea hali hiyo. "Tumeamua kutoa mafunzo haya kwa awamu na kwa kundi hili tunalenga kuwa watakuja kuisaidia jamii katika kudhibiti biashara hii haramu ambayo imekuwa ikiathiri vijana wengi kudanganyika na kwenda kuuzwa nje kwenye madanguro na kwa mfanyabiashara mmoja huwa anatengeneza faida ya Dola 5,000 mpaka 10,000 kwa kichwa, hivyo kutokana na faida hiyo inahitajika juhudi za dhati kudhibiti hili," alisema.

Naye Mwakilishi wa Sekretarieti ya kuzuia na kupambana na usafirishaji wa biashara haramu ya binadamu, Ahmad Mwendadi alisema: "Tumedhamiria kukomesha biashara hii haramu ambayo inawatengenezea faida zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni 150 hivyo lazima tuwe macho na tunaomba ushirikiano kwa jamii ili tufanikishe kudhibiti."

# CBE yajivunia mafunzo ya uanagenzi

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimesema mafunzo ya uanagenzi yamewasaidia wanafunzi wa chuo hicho kuwa na uwezo wa kujiajiri na kuajiri wenzao wanapomaliza chuo.

Pia mafunzo ya uanagenzi yamesaidia kuwapunguzia mzigo waajiri ambao hulazimika kutumia fedha nyingi kuwaendeleza watumishi ambao wanaajiriwa wakiwa bado hawana ujuzi wa kutosha.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Edda Lwoga, wakati wa mkutano wa mameneja rasilimali watu wa kampuni mbalimbali nchini.

Uongozi wa chuo hicho ulikutana na wakuu wa vitengo vya rasilimali watu wa taasisi na mashirika mbalimbali ya serikali na binafsi (HRO's Breakfast), lengo likiwa ni kuimarisha uhusiano baina ya chuo hicho na taasisi zao.

Lengo lingine la kukutana nao ni kupokea michango na marejesho mbalimbali toka kwa maofisa rasilimali watu wa taasisi ambazo huwapokea na kuwaajiri wahitimu wa CBE.

Profesa Lwoga alisema mrejesho huo hutumiwa na chuo kuboresha mitaala na mbinu za ufundishaji ili ziendane na soko halisi la ajira na mahitaji ya ujuzi unaohitajika kwenye ajira.

"Nyinyi ni mashahidi mwanafunzi akihitimu mkamwajiri akiwa hana ujuzi wa kutosha mnatumia fedha nyingi kumwendeleza kupata ujuzi zaidi. Kwa hiyo tumeanzisha programu ya uanagenzi ambapo mwanafunzi anakaa asilimia 50 darasani na asilimia 50 kwa mwajiri na imesaidia sana kuwajengea uwezo kwa vitendo," alisema.

Alisema kupitia programu ya uanagenzi inayofanywa na CBE wanasaidia kwa kiasi kikubwa waajiri kupata wafanyakazi ambao hawahitaji kuendelezwa zaidi kwa kuwa wanakuwa tayari na ujuzi wa kutosha kwenye nyanja zao za utaalamu. "Kwa kufanya hivi tunaamini kwamba tunakwenda na kasi ya awamu ya sita na kuwasaidia waajiri kusumbuka kumwendeleza mwajiriwa wao," alisema. Alisema CBE pia ilianzisha programu atamizi ya mawazo ya biashara kwa wanafunzi wa chuo hicho na imekuwa na mafanikio makubwa tangu ianzishwe.

"Wanafunzi wanakuja wakiwa na ndoto za ubunifu sisi tunawanoa na hatufanyi peke yetu tunashirikiana na SIDO kuwajengea uwezo na mwenye ndoto ya biashara anaweza kuanza kufanya biashara akiwa chuoni tukamuunganisha na masoko na namna ya kusajili biashara," alisema Profesa Lwoga.

Alisema wameanzisha utaratibu wa kuwaita wahadhiri kutoka nje ya chuo hicho waliobobea kwenye biashara kuja kuwapa mihadhara wanafunzi wao. Kadhalika, utaratibu huo umesaidia kwa kiwango kikubwa kuwanoa wanafunzi na kuwapa ujasiri wakimaliza chuo kuwa na uwezo wa kwenda kufanyakazi kwa ufanisi na kuonyesha matokeo mazuri.

Alisema CBE pia imeweka utaratibu wa kuwaendeleza wahadhiri wake kwenye kampasi zake zote nne, walimu ni 215 na watumishi kwa ujumla ni 459.

"Miongoni mwa wahadhiri hao, 30 wamesoma ngazi ya Shahada ya Uzamivu (PhD) na 71 wako masomoni na hii inaonyesha kwamba CBE tuko kwenye njia sahihi kupata watu watakaowapika wahitimu bora," alisema.

# Asilimia 40 wanafunzi wa kike hukosa masomo siku za hedhi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANAFUNZI wa kike 360 kati ya 900 wa Shule ya Sekondari Gairo wa kidato cha kwanza hadi cha sita, wilayani humo mkoani Morogoro wanashindwa kuhudhuria masomo yao kila mwezi wanapokuwa kwenye hedhi kwa kukosa vifaa sahihi vya kujisitiri. Wengi wao hulazimika kutumia njia za asili kwa kushindwa kumudu gharama za kununua taulo za kike.

Kauli hiyo imetolewa na Muuguzi wa Shule ya Sekondari ya Gairo, Moshi Joseph, kwenye kampeni ya kumfikia mtoto wa kike kielimu inayofanywa na Kampuni ya DoweiCare katika shule mbalimbali nchini ambao waligawa bure taulo za SoftCare na za ziada kwa wanafunzi.

Alisema idadi ya wanafunzi wanaoshindwa kuhudhuria masomo ni sawa na asilimia 40 kwa mwezi na wamejikuta wakiathirika kimasomo, kutokana na wengi wao wakati wa hedhi kubaki nyumbani. Kutolewa kwa taulo hizo kutaongeza mahudhurio hayo kila mwezi. Alifafanua kuwa upatikanaji wa taulo hizo mwitikio wa watoto utaongezeka kwa kasi kubwa kwa kuwa awali iliwalazimu wasichana kurudi nyumbani pindi anapopata hedhi akiwa shuleni ama wakati mwingine kushindwa kufika shule kwa siku tatu hadi nne na kumfanya kukosa masomo.

Mmoja wa wanafunzi wa kidato cha tano, Grolia Wilson, alisema wanafunzi wa kike wanapitia changamoto nyingi wanapokosa taulo hizo ikiwamo kushikwa na aibu, kuhofia kuchekwa wanapobainika wapo katika hedhi na kujikuta wakilazimika kukaa nyumbani na kukosa masomo.

Passanen Edwaed wa kidato cha kwanza alisema changamoto nyingine wanayokutana nayo ni kukosa amani wakati wa kujisomea kutokana na kuchanganyika na wanafunzi wa kiume na kusababisha kukosa vipindi vingi na kurudisha nyuma maendeleo yao kimasomo.

Meneja wa Biashara wa Kampuni ya DoweiCare, Lucia Msami, alisema wameamua kusaidia taulo hizo ili kupunguza matumizi ya vifaa hatari kwa wasichana wa kike katika shule hiyo. "Sisi kama DoweiCare tupo tumeamua kumuunga mkono Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika elimu sote tumeona wasichana waliopata mimba amewarudisha shuleni na sisi tumeamua kuwaondolea changamoto za matumizi ya vifaa hatarishi wanapokuwa katika hedhi," alisema Lucia.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabir Makame, alisema kwa sasa wanafunzi wa kike katika maeneo mbalimbali nchini wana nafasi ya kufanya vizuri kitaaluma kutokana na serikali kuondoa vikwazo vingi na kutengeneza mazingira rafiki ya kujifunzia ikiwamo elimu bure, mikopo ya elimu ya juu, maabara kwa masomo ya sayansi na mazingira rafiki ya kujistiri wakati wa hedhi.

Makame alisema serikali haitachoka kuendelea kuwathamini watoto wa kike na hii ni katika kuhakikisha mtoto wa kike anapata elimu. Kampuni hiyo ya DoweiCare pia walitoa msaada wa mahindi kilo 500 na maharage kilo 300, matarajio ni kufikia shule tano, kwa sasa shule tatu za sekondari Mkoa wa Morogoro zimefikiwa ambazo ni Ngerengere, Morogoro Sekondari na Gairo.

# TEMESA watakiwa kuboresha huduma, kupunguza gharama

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella amewashauri Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kuboresha huduma zao, kupunguza gharama ili wadau wa serikali, taasisi na idara zake waifanye kuwa kimbilio la kwanza katika matengenezo ya magari na huduma zingine na kuacha kwenda mitaani.

Mongella aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Arusha, wakati wa ufunguzi wa kikao cha wakala huyo na wadau wake ambao ni idara, taasisi na wakala za serikali.

Alisema huduma zikiboreshwa hakuna mdau atakayekimbilia mtaani, badala yake atakimbilia TEMESA ambao kimsingi walianzishwa ili wadau serikalini waitumie.

"Lakini miaka ya hapo nyuma kulikuwa na changamoto ya utoaji huduma zao, tofauti na sasa kuna maboresho makubwa lakini endeleeni kuboresha ili tuifanye kimbilio letu la kwanza, maana ukipata huduma bora hutakimbilia mtaani,"alisema.

Aidha, aliomba wadau wa TEMESA zikiwamo idara, taasisi na wakala za serikali kumuunga mkono wakala huyo ili nayo iendelee kutoa huduma bora.

Alisisitiza fursa za TEMESA ni kubwa mno sababu katika majengo ya serikali mengi kuna ujenzi wa majengo na kazi mbalimbali zinaendelea, hivyo huduma zikiwa nzuri na kazi watapata nyingi.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi Umeme (TEMESA), Lazaro Kilahala, alisema wakala huyo ni taasisi wezeshi yenye kutoa huduma kwa serikali katika kuleta ufanisi zaidi.

Alisema TEMESA awali ilikuwa haifanyi vema katika matengenezo ya magari ikiwamo gharama kubwa ya ufundi, lakini sasa hivi imeanza kutumia utaratibu mpya wa kupunguza muda wa uagizaji wa vipuri pia kwa kutumia mzabuni.

Pia, aliishukuru serikali kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kukarabati miundombinu yake kwa ajili ya kuhakikisha huduma zao zinakuwa bora na kununua vifaa vya kisasa.

# MoCU kufumua mitaala kuendana na hali halisi

**Na Mwandishi Wetu,**

CHUO Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kimeanza rasmi mchakato wa kukusanya maoni ya waajiri katika bodi zinazosimamia taaluma na utaalamu, sekta ya umma na binafsi, wahitimu na wanafunzi, kabla ya kuifumua mitaala 15 na kuandaa programu mpya 11 zitakazoamua hatima ya wanaohitimu elimu ya juu kukabiliana na soko la ajira. Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Alfred Sife, wakati anazindua mpango huo juzi, alisema hatua hiyo ni muhimu katika kipindi ambacho soko la ajira limebadilika, kwa maana ya kuwa na mahitaji mapya ya ujuzi na maarifa.

Prof. Sife alisisitiza kuwa hatua hiyo inachagizwa pia na mwingiliano wa ajira kwa mataifa mbalimbali kutokana na utandawazi, idadi ya wahitimu kuongezeka kupita uwezo wa nafasi za ajira zinazozalishwa na sekta mbalimbali.

"Tuko katika kipindi kijulikanacho kama mapinduzi ya viwanda yanayoongozwa na matumizi makubwa ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), hivyo kuhitaji uzalishaji wa wahitimu wenye ujuzi na mapinduzi haya,"alisema.

Kabla ya uzinduzi huo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Utawala na Fedha wa MoCU, Prof. Fredy Kilima, alisema maboresho hayo ni utekelezaji wa mradi wa kitaifa wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi.

Mradi huo unaotekelezwa katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, ni sehemu ya vyuo vingine 14 vilivyoko hapa nchini.

"Mradi unafadhiliwa na serikali ya Tanzania chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Dhima kuu ya mradi huu ni kuwa na elimu inayoendana na soko la ajira.

"Kimkakati kuna namna nyingi za kufikia lengo hili ili kutimiza dhima ya mradi mojawapo ya mikakati iliyopendekezwa na mradi, ni kufanya marejeo ya mitaala iliyoko na kuandaa mitaala itakayowawezesha wahitimu kuwa na ufahamu na maarifa yatakayoleta tija kwenye soko la ajira," alisema.

Aidha, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, anayeshughulikia taaluma, utafiti na ushauri elekezi, Prof. John Safari, akizungumzia maboresho hayo, alisema: "Umuhimu wake unaonekana katika elimu tunayoitoa inaakisi mahitaji ya wakati ya kijamii na kiuchumi.

"Tunafanya hivyo ili kuhakikisha kwamba tunajibu hoja ya changamoto mbalimbali za kijamii na kwa hiyo maoni yanapaswa kutoka kwa jamii yenyewe ambayo ni Watanzania wenzetu."



Mkurugenzi wa Kampuni ya Kumburu Sisal Plantation LTD wilayani Muheza mkoani Tanga, Hamisi Kindoroko (kulia), akikabidhi msaada wa mabati 60 yenye thamani ya Shilingi milioni mbili kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Mpapayu wilayani humo mwishoni mwa wiki. Katikati ni Kaimu Ofisa Mtendaji Kata ya Mpapayu, Mwanaidi Mwaimu, akipokea mabati hayo na Meneja Uzalishaji wa kampuni hiyo, Waziri Kingazi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Samia amaliza mgogoro kati ya wakazi vijiji 5, KIA

**Na Mary Mosha,** MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameumaliza rasmi mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa vijiji vitano vinavyopakana na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), baada ya kukubali kuwalipa wakazi hao fidia ya Sh. 11.3 ili kupisha eneo hilo.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 7.3 zitalipwa kwa wananchi wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro na Sh. bilioni 4.04 zitalipwa kwa wananchi wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.


Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alieleza Nipashe mwishoni mwa wiki kwamba, wananchi hao wanamshukuru Rais Samia, kwa upendo wake wa kushughulikia na kuumaliza mgogoro huo kwa muda mfupi.

Eneo la uwanja huo lililokuwa likikaliwa na wananchi hao na ambalo limefanyiwa kutokana na mgogoro huo, lina ukubwa wa zaidi ya hekta 11.4.

Aidha, vijiji vitakavyolipwa fidia kutokana na mgogoro huo wa mipaka kati yake na Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO), ni Chemka, Rundugai, Sanya Station, Tindigani na Mtakuja.

Katika taarifa hiyo ya mkoa, inaelezwa kuwa eneo hilo lilitengwa kimkakati na serikali, likiwa na hati ya umiliki wa ardhi ya miaka 99.

Kwa mujibu wa Babu, kutokana na tathmini iliyofanyika, imebainika kuwa wako wananchi walioingilia eneo la uwanja kinyume na taratibu, lakini wananchi hao wa Arusha na Kilimanjaro watalipwa fidia ili kuwasaidia kuendelea na shughuli zao za kiuchumi.





# Mradi kumaliza tatizo la udumavu, utapiamlo kwa wanafunzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI 120,000 kutoka shule za msingi za mikoa sita ya Kanda ya Ziwa wanatarajia kuondokana na udumavu pamoja na utapiamlo kupitia mradi wa uhamasishaji ulaji wa vyakula vilivyoongezwa virutubishi.

Wanafunzi wanaotarajiwa kufikiwa na mradi hao ni kutoka mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga, Kagera pamoja na Simiyu.

Mradi huo unatekelezwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Shirika la GAIN na Kampuni ya SANKU kwa Sh. milioni 910.

Akieleza utekelezaji wake, Meneja Mradi kutoka shirika hilo, Archard Ngemela, wakati wa kikao cha utambulisho wa mradi kilichofanyika wilayani Kahama alisema watawafikia wanafunzi 120,000 katika shule za msingi 240.

Alisema wanafunzi hao watakula vyakula vilivyongezewa virutubishi lishe kwa kushirikiana na wazalishaji wa unga 75 katika mikoa hiyo, lengo likiwa ni kupambana na tatizo la utapiamlo na udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

"Kamati za shule kwa kushirikiana na wazazi wanatakiwa kununua unga uliongezewa virutubishi kwa wazalishaji wanaongeza virutubishi, maofisa afya na lishe watakuwa na jukumu la ukaguzi wa vyakula shuleni,"alisema Ngemela.

Kaimu Mkurugenzi wa Lishe kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mwita Waibe, alisema ni asilimia 47 ya watoto wadogo nchini wapo vizuri kiafya, huku asilimia 53 wanatatizo la utapiamlo na 30 wana udumavu.

Alisema mwaka 2015/2016 watoto milioni 2.9 walikuwa na udumavu mkubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema mjamzito anapopata lishe bora anaondokana na kuzaa mtoto jinti na mgongo wazi.

Alisema Mkoa wa Geita unaongaza kuwa na watoto wenye utapiamlo kwa asilimia 38.6 ikifuatiwa na Kagera (34.2), Simiyu (33.2), Mwanza (27.9), Shinyanga (27.5) Mkoa wa Mara (23.2) na kuwataka maofisa lishe kusimamia suala la kuongeza virutubishi katika vyakula shuleni.

# CPB yatoa tani moja ya mchele shule ya msingi

**Na Vitus Audax** MWANZA

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) Kanda ya Ziwa imetoa tani moja ya mchele katika Shule ya Msingi Butimba A kwa lengo la kuboresha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi na kupunguza adha ya wazazi kuchangia chakula shuleni.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Kaimu Meneja wa CPB Kanda ya Ziwa, Alfred Klimenze, alisema wataendelea kutekeleza mpango wa serikali wa kuboresha lishe kwa watoto kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata lishe bora na kukuza kiwango cha elimu hasa wawapo darasani.

Kadhalika alizitaka kamati za shule za chakula kuendelea kuwashirikisha katika mahitaji yao ya chakula ili kuweza kuona njia sahihi za kuchangia huduma hiyo kwa wanafunzi ikiwa ni sehemu ya mpango wa bodi hiyo kurudisha kwa jamii.

Aidha, aliwataka walimu kutengeneza mfumo rafiki kupitia kwa walimu wakuu ili kuweza kufika katika ofisi za bodi hiyo ya nafaka na kuweza kukopeshwa nafaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na mchele.

Naye Ofisa Elimu Msingi na Awali wa Jiji la Mwanza, Mussa Ally, aliwataka wazazi kuacha kuitafsiri vibaya sera ya elimu bila malipo kwa kugoma kuchangia huduma mbalimbali zikiwamo za chakula cha wanafunzi walioko shuleni na kuitupia mzigo huo serikali.

Alisema hali hiyo inayosababisha wanafunzi wengi kushindwa kumudu masomo kutokana na kukosa chakula na kuchochea utoro shuleni.

Kati ya shule 80 za msingi zilizopo jijini Mwanza ni shule 20 pekee zinatoa uji kwa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza, shule 14 zinatoa huduma ya chakula kwa madarasa ya mitihani.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, akipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa kampuni ya SANKU kuhusu mtambo wa kuongeza virutubishi kwenye nafaka unavyofanyakazi. Nyuma yake ni Mwita Waibe, Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Afya na Lishe TAMISEMI. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shinyanga yajivunia uboreshaji afya miaka 2 ya Samia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imesema katika miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan wameimarisha huduma za afya ikiwamo upatikanaji wa dawa uliofikia asilimia 89.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliyasema hayo wakati wa kongamano la miaka miwili ya mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan mkoani humo.

Alieleza kuwa huduma zilizoboreshwa katika mkoa huo ni pamoja na ujenzi wa hospitali, vituo vya afya, zahanati pamoja na upatikanaji wa dawa muhimu za binadamu ambao umefikia asilimia 89.

"Katika sekta ya afya zimetolewa Sh. bilioni 32.6 kwa ajili ya kujengwa vituo vya afya na zahanati, pia akatoa Sh.bilioni 7.8 kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufani mkoani hapa na ameondoa adha ya wananchi kufuata matibabu ya kibingwa nje ya mkoa,"alisema Mndeme.

Kadhalika alieleza kuwa zimetolewa Sh.bilioni 14.9 zilizotumika katika kununua vifaa tiba, dawa.

Aidha, alieleza kuwa mafanikio mengine ni katika sekta za elimu, maji, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara na Reli ya Kisasa (SGR) unaotekelewa mkoani humo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alisema katika kipindi cha miaka miwili ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imeendelea kutekelezwa kwa vitendo, hivyo kuomba kasi iendelee katika kipindi kilicho salia.

Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, alisema fedha zinazoendelea kutolewa na serikali katika utekelezaji wa miradi ya serikali ziendelee kutumiwa vyema na kuepusha ubadhirifu wa aina yoyote.

Nipashe
# Spotika




WANASOKA WA5 WANAOFANANA KIUCHEZAJI NA RONALDO UK. 12-13




ARSENAL

# KLABU 4 ULAYA ZENYE KIWANGO CHA KUSHANGAZA MSIMU HUU

**LONDON,** England

MSIMU wa soka wa 2022-23 umekuwa wa kushangaza na mabadiliko yasiyotarajiwa katika kila ligi.

Wakati baadhi ya timu za soka zimetimiza matarajio yao kabla ya msimu mpya, zimevuka muda wote na zinang'aa zaidi kuliko hapo awali. Timu hizi zimewachanganya wakosoaji na kuweka mazingira ya kumaliza msimu wa kusisimua.

Katika haya, tunaangalia kwa karibu timu nne bora ambazo zimekuwa na uwezo wa kustajabisha msimu huu hadi katikati ya Machi 2023...

**#4 Newcastle United**

Mnamo mwaka 2017, Newcastle United ilipandishwa daraja na kurejea Ligi Kuu Engand baada ya mwaka mmoja kutokuwapo kwa kushuka daraja. Klabu imeonesha maendeleo makubwa katika nyanja ya michezo na kiuchumi.

Kutokana na mauzo ya klabu hiyo kwa Waarabu, matokeo chanya kuonekana msimu huu kuwa wazuri kwa kiwango cha Ligi Kuu England.

Wachezaji kadhaa muhimu wametoa uchezaji bora, haswa katika safu ya ulinzi. Ukiangalia jedwali la sasa la Ligi Kuu England, Newcastle wameshinda michezo 12, sare 11, wamepoteza tatu na wameruhusu mabao 19 pekee, idadi ndogo zaidi kwenye ligi.

Kwa sasa wanashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi na wako mbioni kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao. Wanaweza hata kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa timu mbili zilizo juu yao zitateleza.

**#3 Napoli**

Katika hatua hii ya Ligi Kuu Italia, Serie A, Napoli ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa. Timu hiyo iko mbele ya Lazio iliyo nafasi ya pili kwa pointi 19.

Kwa maana jinsi Napoli wamekuwa wazuri msimu mzima, hakuna uwezekano wa kushuka kwa uongozi wao hivi karibuni. Wachezaji kama Osimhen, Kvaratskhelia, Zielinski na Anguissa wameongoza safu ambayo imeifanya Napoli kuwa kileleni mwa Serie A.

Hakuna aliyeona hili likija kwani Napoli ilikuwa timu ya juu ya wastani kwa muongo mmoja uliopita. Kwa kweli, wameshinda Serie A mara mbili tu mwaka 1987 na 1990 wakati Diego Maradona akiwa anawachezea. Kwa sasa wako kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#2 Arsenal**

Kila shabiki wa Arsenal amekuwa akingojea wakati huu kwa miaka mingi. Klabu hiyo ya London Kaskazini ilipata enzi yao yenye mafanikio zaidi miaka ya 2000 chini ya Arsene Wenger.

Tangu walipotwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mwaka 2004 bila kupoteza, kombe hilo halijawafikia tena. Hadi sasa wameweza kushinda Kombe la FA na Ngao ya Jamii na wametolewa kwenye Ligi ya Europa.

Arsenal wamedumisha subira kwa kocha wa sasa, Mikel Arteta na wameanza mavuno ya matunda ya klabu kwa ufanisi. Wanapewa nafasi kubwa ya kushinda taji la Ligi Kuu baada ya takribani miaka 20.

Uchezaji wao msimu huu umekuwa wa kustaajabisha, ikiwa ni pamoja na ushindi wa dakika za majeruhi. Hata hivyo, wakosoaji wengine bado wanawaita "Tembo walioketi kwenye tawi la mti", wakiwa na maana wanatarajia kuona wakianza kupata matokeo mabaya hivi karibuni.

**#1. Union Berlin**

Huenda wengi hawajaona maendeleo yao, lakini Union Berlin imekuwa ya kusisimua kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Timu hiyo inatukumbusha mafanikio ambayo Leicester City ilipata miaka miwili baada ya kupandishwa daraja hadi Ligi Kuu England.

Union Berlin kwa sasa ipo katika nafasi nne za juu za Bundesliga na imekuwa ikionesha uwezo wa hali ya juu. Kati ya 2009 na 2019, timu hiyo ilishiriki kwenye daraja la pili la soka Ujerumani.

Lakini mwaka 2019, Union ilikamilisha kazi ya kihistoria kwa kupata kiwango cha kupanda Ligi Kuu.

Mnamo 2022, walifuzu kwa Ligi ya Europa League matarajio yanaongezeka kwani wengine wanatarajia kuendelea kujiondoa na hata kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## ISIKUPITE

Erling Haaland ni kama yupo dunia yake mwenyewe ya soka. Kabla ya mapumziko ya Kalenda ya Fifa, amefunga mabao nane katika mechi mbili, lakini kwa msimu huu ameshatupia hat-trick sita huku akiwa na jumla ya mabao 42 aliyoifungia Manchester City hadi sasa msimu huu katika mashindano yote.





MBAPPE

# WANASOKA WATANO WANAOFANANA KIUCHEZAJI NA RONALDO

**LONDON,** England

CRISTIANO Ronaldo ni mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote. Alianza kung'ara mapema miaka ya 2000 kama winga mwenye ujuzi mwingi wa mchezo huo. Kwa sababu ya kujitolea kwake kabisa, nidhamu na bidii, alifurahia kupanda kwa haraka kwenye kilele cha ubora.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, ana mtindo wa kucheza sahihi na inaonekana wazi jinsi anavyocheza, chenga au kupiga mipira ya adhabu.**

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or bila shaka amekuwa kivutio cha wanasoka wengi. Kumwiga mwanasoka unayempenda ni jambo la kawaida sana.

Wanasoka chipukizi wanajaribu kuiga mchezo kwa wanasoka wanaowapenda.

Hapa tunwaangalia wanasoka watano ambao wana mtindo wa uchezaji sawa na Cristiano Ronaldo, twende sasa...

**#5 Son Heung-Min (Tottenham Hotspur)**

Son Heung-Min ni mojawapo wa vipaji vya hali ya juu kwa kizazi chake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini amekuwa mmoja wa washambuliaji thabiti katika Ligi Kuu England kwa miaka kadhaa sasa. Son alishinda Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu msimu uliopita kwa pamoja na Mohamed Salah wa Liverpool.

Mtindo wa uchezaji wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, unafanana kabisa na ule wa Ronaldo. Yeye yuko moja kwa moja na mpira miguuni mwake na anapenda kuwafuata mabeki na kuwapiga chenga. Kama Ronaldo katika siku zake za ujana, Son anacheza kama winga wa kushoto ambaye anaweza kupiga mpira kwa miguu yote miwili.

Alijiunga na Spurs mwaka 2015, akitokea Bayer Leverkusen kwa kitita cha euro milioni 30. Kwenye mechi 348 katika mashindano yote kwa miamba hao wa London Kaskazini, Son amefunga mabao 137 na kutoa asisti 76.

**#4 Memphis Depay (Barcelona)**

Kama Ronaldo, Memphis Depay, aliwasili Manchester United akiwa winga mchanga ambaye alikuwa na uwezo wa kuwa mshindi wa dunia. Hakuwa na nafasi nzuri kabisa Old Trafford, lakini alionyesha kung'ara kwa uwezo wake wakati alipokuwa huko.

Ilikuwa kule Olympique Lyon ambapo Depay alifanikiwa kujiimarisha kama fowadi wa ubora wa juu. Ustadi wa Mholanzi huyo wa kucheza chenga ni wa kustaajabisha na unamkumbusha sana Ronaldo wakati wa miaka yake kuu. Yeye pia ni bora katika upigaji mashuti kutoka winga na pia ni mpigaji mzuri wa mipira iliyokufa 'free-kick'.

Kutokana na hali hiyo, uchezaji wa Depay mara nyingi umekuwa ukifananishwa na ule wa Ronaldo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kwa sasa hapewi nafasi sana kule Barcelona kwani Wakatalunya hao wana utajiri katika idara ya ushambuliaji.

**#3 Joao Felix (Chelsea)**

Joao Felix ana mtindo wa kucheza unaofanana kabisa na Ronaldo. Ingawa Ureno imetoa washambuliaji wengi wenye vipaji katika miaka ya hivi karibuni, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anatajwa kama ana siku bora zaidi zinazokuja.

Furaha ilikuwa kubwa kiasi kwamba Atletico Madrid ilimsajili Felix kutoka Benfica mwaka 2019 kwa kitita cha euro milioni 126. Kwa kawaida hutumika kama mshambuliaji wa pili katika mfumo wa Diego Simeone. Ubora wa Felix upo kwa wote kuona, lakini makubaliano yanaonekana kuwa labda Simeone si kocha sahihi kwake.

Sasa amejiunga na Chelsea kwa mkataba wa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu. Felix ni gwiji wa mbele mwenye sifa bora za kiufundi. Uchezaji wake wa kuchezea, ubunifu na upigaji mashuti unaonekana kama ule wa Ronaldo.

**#2 Marcus Rashford (Manchester United)**

Marcus Rashford kwa sasa anacheza katika ubora wake. Kwa kiwango cha sasa, yeye ni mmoja wa washambuliaji bora duniani. Ustadi wake wa kuchezea chenga ni wa hali ya juu na kasi yake ya kusisimua inamruhusu kumpita karibu kila beki anayekutana naye.

Rashford amekuwa Manchester United tangu akiwa na umri wa miaka saba na ni wazi ametengeneza mchezo wake baada ya gwiji wa klabu hiyo, Ronaldo. Mwingereza huyo ni mmoja wa wapiga chenga waliobobea zaidi kwenye sayari hii na hata mara kwa mara anatumia staili ya Ronaldo kuwavaa wapinzani.

Mara nyingi anatumia mbinu ya kupiga chenga na kupiga mipira ya adhabu na ni mtindo ambao ulipendwa na Ronaldo.

**#1 Kylian Mbappe (Paris Saint-Germain)**

Kylian Mbappe ndiye mshambuliaji bora zaidi duniani kwa sasa. Alishinda Kiatu cha Dhahabu kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022 na hata alifunga hat-trick katika fainali ya mashindano hayo. Mbappe alifichua katika mahojiano na Marca mwaka 2017 kwamba Ronaldo alikuwa kipenzi chake utotoni na kwamba alionekana kuiga mtindo wake wa kucheza akiwa mtoto.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, anapendekezwa kufikia au hata kuvuka urithi wa shujaa wake huyo wa utotoni. Kasi yake ya kusisimua na uwezo wa kupiga mashuti humfanya kuwa fowadi hatari sana. Ni ndoto ya kujilinda dhidi yake na ni mmoja wa wachezaji wanaotafutwa sana kwenye mchezo hivi sasa.

## Nukuu

"Mambo mengi lazima yabadilike ili kurejea kwa Leo Messi Barcelona. Kwanza, anatakiwa kupunguza sana mshahara wake; klabu lazima iwatoe wachezaji na mambo mengine ambayo bado hawajayafanya. Ni wao pekee wanaoweza kufanya hivyo. hatutabadilisha sheria. Messi hawezi kuwa Barcelona ama PSG msimu ujao. Kwa hakika, PSG wanaingiza pesa kidogo kuliko Barcelona," **Rais wa La Liga, Javier Tebas, kuhusu Messi ambaye mkataba wake na PSG unamalizika majira haya ya joto na bado hawajafanya mazungumzo yoyote.**



"Jambo moja ninalopaswa kusema - ushauri wangu kwa Arsenal ni kwa Bukayo Saka kusajiliwa kwa miaka 10! Kosa moja ambalo Arsenal walifanya kwa miaka mingi, walikuwa na wachezaji muhimu ambao waliipenda klabu na wakawaacha waondoke. Ni lazima ubaki na wachezaji hao, kwa sababu ndio watakaoongoza timu kwa ajili yako," **Beki wa zamani wa Arsenal, Muivory Coast Kolo Toure, akitoa ushauri wake kwa 'Gunners' ya Mikel Arteta.**



"Nilikuwa nikijadili hili na Casemiro, Vinicius Junior, (Eder) Militão. Kuna uwezekano mkubwa kwamba [Carlo Ancelotti] atakuja, ni kocha wa kipekee, kila mtu katika kundi lake anampenda ni mtu wa ushindi, angalia tu CV yake. Tutajua baada ya muda mfupi kama atakuwa hapa au la," **Kipa wa Brazil na Manchester City, Ederson, kuhusu Ancelotti kuinoa timu yao ya taifa.**





CRISTIANO Ronaldo ni mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote. Alianza kung'ara mapema miaka ya 2000 kama winga mwenye ujuzi mwingi wa mchezo huo. Kwa sababu ya kujitolea kwake kabisa, nidhamu na bidii, alifurahia kupanda kwa haraka kwenye kilele cha ubora.

Uk. 12&13




Washambuliaji wa Yanga waliyoipeleka robo fainali Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu kwa mabao yao dhidi ya US Monastir ya Tunisia wakati wakishinda 2-0, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: YANGA SC**

# YANGA NA REKODI YA MIAKA 28 ROBO FAINALI SHIRIKISHO AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni siku ya kihistoria kwa wanachama, mashabiki wa Yanga baada ya klabu yao kutinga hatua ya robo fainali kwa mara ya kwanza kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Baada ya kipenga cha mwamuzi kupulizwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Machi 19, mwaka huu, ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya US Monastir ya Tunisia, iliashiria kuwa klabu hiyo kongwe imeweka rekodi ya kutinga hatua hiyo kwenye kombe hilo tangu lianzishwe miaka 19 iliyopita.

**Ikumbukwe kombe hilo lilianzishwa kwa mfumo huu wa sasa ambao unaanzia mtoano hadi makundi, baada ya ule wa mwanzo ambao ni mtoano hadi mwisho.**

Kombe la Shirikisho barani Afrika lilianzishwa mwaka 2004, likichukua nafasi ya Kombe la CAF lililoanzishwa mwaka 1992 ambalo Simba iliingia fainali mwaka 1993 na kufungwa na Stella Abdijan mabao 2-0, likibadilishwa mfumo na kuuweka huu ambao leo tunaouona, tofauti na ule wa awali ambao ni washindi wa pili tu wa ligi ya nchi wanachama husika ambao walikuwa wakishiriki.

Kombe la CAF, ambalo lilijulikana sana kama Kombe la Abiola, likipewa jina la mfanyabiashara tajiri na mwanasiasa wa nchini Nigeria, Mashood Abiola.

Kabla la kuitwa hivyo lilijulikana kama Kombe la Washindi barani Afrika, ambapo pia washiriki wake ni timu zile zile zilizokuwa zikikamata nafasi ya pili kwenye nchi wanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (CAF), lilichezwa na mtindo ule ule wa mtoano mwanzo mwisho.

Kombe la Washindi lilianzishwa miaka 1975 na ndilo asili ya Kombe la Shirikisho tunaloliona leo, CAF wakilibadisha majina na mifumo kwenda Kombe la CAF na baadaye Shirikisho kutokana na mahitaji na mazingira.

Historia inaonesha kuwa Yanga imeshawahi kutinga robo fainali ya Kombe la Washindi mwaka 1995, na imesotea hatua hii kwa miaka 28 sasa.

Lakini haijawahi kutinga hatua ya robo fainali tangu lilipoanza kuitwa Kombe la CAF hadi Kombe la Shirikisho takriban miaka 30 iliyopita hadi mwaka huu ilipofanya hivyo.

Ilifanya majaribio kadhaa na kufanikiwa kutinga hatua za makundi, ilishindwa kutinga hatua ya robo fainali mara mbili 2016 na 2018 ilipofanikiwa kucheza hatua ya makundi, lakini ikiishia kukamata mkia.

**Ilivyotinga robo fainali Kombe la Washindi**

Miaka 30 iliyopita, Yanga ilicheza robo fainali ya Kombe la Washindi, ilipoanza raundi ya kwanza kwa kuifunga Vaal Professional ya Afika Kusini jumla la mabao 4-3, ikitoa sare ya mabao 2-2 ugenini na kushinda nyumbani 2-1 na mechi ya raundi ya pili ilicheza dhidi ya Cadets Club ya Mauritius, ikafanikiwa kushinda kwa jumla ya mabao 4-2, ikishinda nyumbani 3-1 na kulazimisha sare ya bao 1-1 ugenini na kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali mwaka 1995.

Hata hivyo, ilitolewa kwenye hatua hiyo kwa kuchapwa jumla ya mabao 4-2 dhidi ya Blackpool FC ya Zimbabwe, ikifungwa mabao 2-1 mechi zote mbili, nyumbani na ugenini.

**Jaribio lililoshindikana mwaka 2016**

Yanga ilitinga hatua ya makundi mwaka 2016, ikiitafuta robo fainali yake ya kwanza tangu kuanza kwa mfumo mpya wa Kombe la Shirikisho. Ilikuwa kwenye Kundi A, pamoja na timu za TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Mo Bejaia ya Algeria na Medeama ya Ghana.

Haikufanikiwa, kwani ikiishia kukamata mkia kwenye kundi ikimaliza na pointi nne, ilizozipata kwa kuifunga Mo Bejaia bao 1-0 nyumbani na sare ya bao 1-1 dhidi ya Medeama Dar es Salaam, huku ikipoteza mechi nne, mabao 3-1 ugenini dhidi ya TP Mazembe na Medeama, bao 1-0 dhidi ya Mo Bejaia ugenini na idadi kama hiyo dhidi ya TP Mazembe nyumbani.

**Ikashindwa tena mwaka 2018**

Ilishindwa kwa mara ya pili kutinga hatua hiyo mwaka 2018, ilipotingia hatua ya makundi. Ikiwa kwenye Kundi D, safari hii ilikuwa pamoja na USMA Alger ya Algeria, Rayon Sports ya Rwanda, na Gor Mahia ya Kenya.

Kama mwaka 2016, ilimaliza ikiburuza mkia kwenye kundi hilo, ikiwa pia na pointi nne ilizozipata kwa kuifunga USMA Alger mabao 2-1 nyumbani, na suluhu dhidi ya Rayon Sports, huku ikipoteza mechi nne, ikichapwa nyumbani mabao 3-2 dhidi ya Gor Mahia, ugenini mabao 4-0, na idadi kama hiyo ya mabao dhidi ya USMA Alger, bao 1-0 dhidi ya Rayon Sports.

**Historia imeandikwa 2023**

Hatimaye mwaka huu, Yanga ikafanikiwa kutimiza azima yake ya kucheza robo fainali baada ya kushindikana miaka yote hiyo.

Kama ilivyokuwa mwaka 2018, ilipangwa Kundi D, pamoja na mechi ya kwanza kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya US Monastir ugenini, ilirekebisha makosa, ikaifumua TP Mazembe 3-1 nyumbani, ikaenda kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Real Bamako ugenini kabla ya kuifunga nyumbani mabao 2-0 na kisha kupata ushindi wa mabao 2-0 nyumbani dhidi ya US Monastir.

**JE, WAJUA?**



WINGA na nahodha wa Real Betis, Joaquin (41) na Kipa wa Rayo Vallecano, Diego Lopez (41), ndio wachezaji wenye umri mkubwa zaidi katika Ligi Kuu Hispania, LaLiga kwa sasa, wakifuatiwa na mlinda mlango wa Villarreal, Pepe Reina (40), Kipa wa Real Betis, Claudio Bravo (39) na Kiungo wa Real Madrid, Luka Modric, 37.



# Mfuko wa Self watoa bil.313/- kwa wajasiriamali 225,000

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MFUKO wa Self Microfinance Fund uliopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambao una jukumu la kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wenye kipato cha chini umetoa mikopo ya Sh.bilioni 313 kwa wanufaika 225,000.

Meneja Masoko na Uhamasishaji wa mfuko huo, Linda Mshana, akizungumza juzi wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Singida na Dodoma alisema mikopo hiyo imetolewa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi 2022.

Alisema mikopo hiyo yenye masharti nafuu imetolewa kwa wajasiriamali wadogo, taasisi za fedha, benki za kijamii na Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) na kwamba mfuko ulianza na mtaji wa Sh. bilioni 62 lakini kutokana na marejesho mazuri ni takribani asilimia 93 mtaji wa mfuko umefikia Sh. bilioni 313.

Mshana alisema jukumu la SELF ni kuwapa watu fursa ya kufanya kazi kupitia utoaji wa huduma za mikopo midogo kwa gharama nafuu, kwamba mikopo inayotolewa ni ya kilimo, biashara, makazi, ada, mshahara na mikopo kwa vikundi.

Meneja wa Tawi la Dodoma, Aristid Tesha, alisema mikopo inayotolewa na mfuko huo inakuwa na bima isipokuwa ile inayotolewa kwa kampuni na kwamba bima inayotozwa kwa mteja ni asilimia 0.6 kwa mwaka.

Tesha alisema mikopo inatolewa kwa wale wanaofanya biashara ambazo siyo haramu na kwamba huduma zinazotolewa na mfuko huo ni mafunzo kwa taasisi za fedha, kuzisaidia taasisi kutengeneza na kuanzisha mifumo ya fedha na kutoa elimu ya fedha na mikopo kwa jamii nzima.

Mmoja wa wanufaika wa mikopo inayotolewa na SELF, Aziza Nasibu, ambaye ana kiwanda cha kuchakata chupa za maji, alisema alianza biashara hiyo kwa kuokota chupa mitaani kwa kushirikiana na mume wake na walikuwa wakisafirisha kupeleka Dar es Salaam.

Alisema baadaye alikutana na maofisa wa Mfuko wa SELF na kukopa Sh. milioni 50 na hivi sasa amefungua viwanda vitatu, viwili vipo mkoani Dodoma na kimoja mkoani Dar es Salaam.

# TMA yawataka wakulima kuzingatia ushauri wa wataalamu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imewataka wakulima nchini kuzingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo ili kulima mazao yanayostahimili mabadiliko ya hali ya hewa na uchache wa mvua.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Ladislaus Chang'a, alibainisha hayo juzi jijini hapo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani.

Alisema wakulima wanapaswa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo na kuzingatia taarifa ambazo zinatolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kulima kilomo chenye tija kutokana na kiasi cha mvua kilichopo.

"Leo (juzi) Tanzania inaungana na nchini nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani lakini nitumie fursa hii kuishukuru serikali yetu kwa uwekezaji mkubwa uliofanyika ikiwamo ununuzi wa rada."

"Hali hii imetufanya sisi kuwa moja ya nchini ambazo zinaaminika kwenye ufanisi wa taarifa za utabiri wa hali ya hewa kwa kuwa na ufanisi wa asilimia 86 zaidi ya kiwango kilichowekwa na Shirika na Kimataifa la Hali ya Hewa Duniani,"alisema.

Alisema kutokana na ufanisi ulipo hivi sasa kwenye mamlaka hiyo wakulima hawana budi kuzitumia taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa na TMA ili kuwa na tija kwenye kilimo.

Alisema hivi sasa mamlaka hiyo ina rada saba ambazo zimefungwa na nyingine zitarajiwa kufungwa hivi karibuni ili kuendelea kuongeza ufanisi katika taarifa na utabiri wa hali ya hewa.

"Hivi sasa uwezo tulionao tunaweza kutabiri kitu ambacho lazima kitatokea kama mvua za Machi 21 Dodoma tulitabiri na kweli zilitokea vilevile hivyo wakulima wanapaswa kuendelea kutumia taarifa zetu ili ziwasaidie kwenye kilimo," alisema.

Aidha, alisema mamlaka hiyo inaendelea kutoa elimu kwa umma ili kuijengea uelewa jamii wa kutumia taarifa za utabiliwa wa hali ya hewa na kujilinda na majanga mbalimbali.

Hata hivyo, alisema taarifa za hali ya hewa zina manufaa katika sekta nyingi ikiwamo kilimo, ujenzi, uchukuzi ambapo zikitumia vizuri zinamchango mkubwa kwenye ukuaji wa pato la taifa.




Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Zacharia Mwansusa, akizungumza na wadau wa kilimo katika hafla ya kuhamasisha ukuaji wa kampeni ya Kijanisha Maisha chini ya Taasisi ya PAss Trust mkoani Tabora, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aruhusu machinga kufanya kazi saa 24

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wafanyabiashara wa soko la kisasa la machinga jijini Dodoma kufanya kazi kwa saa 24 ili kukuza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla.

Aidha, amezitaka baadhi ya benki kutumia fursa zilizopo kwenye soko hilo kwa kufungua mashine za kutolea fedha ili kuwarahisisha wafanyabiashara kutoa na kuhifadhi fedha zao.

Senyamule aliyasema hayo jana baada ya kupokea maandamano ya wafanyabiashara wa soko la machinga ya kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kutokana na kuelekeza wafanyabiashara wadogo wadogo (machinga) kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira mazuri ili kukopesheka.

Alisema moja ya matarajio ya viongozi wa Mkoa wa Dodoma ni kuona soko hilo linapiga hatua na kuchangia machinga kutimiza azma ya Rais ya kutaka wafanyabiashara hao kufanya kazi katika mazingira wezeshi.

"Tunamshkuru sana Rais kutokana na kuwawezesha machinga wa soko hili kufanya biashara zao katika mazingira mazuri, imewasaidia kusonga mbele kutokana na mikopo wanayopata," alisema.

Senyamule alisema nchi imekuwa ikihangaika na kundi hilo kwa muda mrefu lakini hivi sasa linafuraha na amani ikiwamo kuendesha shughuli zake bila bugudha yoyote.

"Nawapongeza sana machinga wa Dodoma kwa kuonyesha utofauti, na huu ni mfano wa kuigwa kila mahali kwa kuona jitihada zinazofanywa na serikali," alisema Senyamule.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Machinga mkoani hapo, Christian Msumari, alisema miaka miwili ya Rais imewapa fursa nyingi machinga ya kufanya biashara zao bila bugudha yoyote katika eneo maalumu la soko ambalo wametengewa.

Aliishukuru serikali kutokana na kuwawezesha wafanyabiashara hao kutambulika katika maeneo mbalimbali, ikiwamo kuwaweka katika wizara ya maendeleo ya jamii, jambo lililochangia wao kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza biashara zao. "Hivi sasa machinga tunatambulika katika wizara mbalimbali hapa nchini, hii imetusaidia sana, tunamshukuru Rais kwa kutuwezesha hilo," alisema Msumari.

Awali, Mkuu Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwaongeza machinga hao kutokana na kufanya maandamano yenye amani ya kutambua mchango unaofanywa na serikali. Alisema soko hilo ni utalii wa ndani, hivyo wanapaswa kulisimamia vizuri ili kutoa mapato mengi.





# Kampuni kutoka Dubai yatoa msaada wa vyakula msikitini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMPUNI ya usafirishaji na uendeshaji wa bandari mbalimbali duniani iitwayo DP World yenye makao makuu yake Dubai, imetoa msaada wa vyakula kwa waumini wa dini ya kiislamu jijini Mbeya wanaotoka kwenye familia zisizokuwa na uwezo.

Msaada huo umetolewa kwa ajili ya kuzisaidia familia hizo kuandaa futari katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao waumini wa dini hiyo nchini wanaungana na wenzao duniani kutimiza moja ya nguzo kuu za uislamu.

Meneja wa Kitengo cha Misaada na Utawala wa Kampuni hiyo, Salem Almansoori, alikabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki kwa waumini wa Msikiti wa Ul Jumaa uliopo Sokomatola jijini Mbeya ambao ni miongoni mwa misikiti miwili nchini ya kwanza kunufaika na msaada huo.

Almansoori alisema kwa Tanzania msaada huo wanatoa katika misikiti miwili ambayo mmoja upo Tanzania Bara (Mbeya) na mwingine upo Tanzania Visiwani. Alisema kampuni hiyo inafanya kazi katika mataifa 50 duniani, huku mataifa 10 kati yake yakiwa barani Afrika na kwamba kwa Tanzania wanakusudia kufungua ofisi hivi karibuni.

Alisema msaada waliotoa ni sehemu ya faida ambazo kampuni hiyo inapata kutokana na biashara na uwekezaji wake kwenye shughuli mbalimbali za usafirishaji. "Tumeanzisha kitengo maalumu cha misaada ambacho kinaitwa DP World Foundation ambacho kazi yake ni kutoa misaada kwa wahitaji, kwa Tanzania ni mara ya kwanza kufanya kitu kama hiki lakini kutokana na namna tulivyopokelewa vizuri tutakuwa tunafanya hivyo kila mwaka," alisema Mansoori.

Alisema mbali na msaada huo pia wataendelea kushirikiana na waumini wa msikiti huo ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye ujenzi wa msikiti mpya ambao umeanza katika eneo hilo.

Mwakilishi wa kampuni hiyo nchini, Emmanuel Kakuyu, aliwataka Watanzania kuendeleza ushirikiano uliopo bila kujali tofauti ya dini zao ili kuendeleza amani na mshikamano.

Alisema yeye ni mkristo anayesali Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) lakini viongozi wa kampuni hiyo walimpa uhuru wa kuchagua misikiti ya kuisaidia hapa nchini na ndipo akachagua msikiti huo wa UL Jumaa uliopo Mbeya.

Alisema Waislamu na Wakristo wote wanamwabudu Mungu mmoja na hivyo hakuna sababu ya kutoshirikiana kwa sababu ya tofauti ya dini hizo mbili.

Baadhi ya wanufaika wa msaada huo waliwashukuru viongozi wa kampuni hiyo kwa kuwakumbuka wakieleza kuwa walikuwa hawana mwelekeo mzuri wakati huu wa mfungo.

Mmoja wa wanufaika hao, Ania Stambuli alisema msaada huo utawasaidia kufunga na kuswali kwa imani katika kipindi chote cha mwezi mtukufu.



Viongozi wa kampuni ya usafirishaji na uendeshaji wa bandari mbalimbali duniani ya DP World Foundation yenye makao makuu yake Dubai wakiwakabidhi waumini wa dini ya Kiislamu wa Msikiti wa Ul Jumaa uliopo jijini Mbeya futari kwa kaya zisizokuwa na uwezo kwa ajili ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## 'Wazazi wachunguzeni watoto kuwabaini kama wana usonji'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZAZI na walezi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameshauriwa kuwafanyia uchunguzi wa mara kwa mara watoto wenye umri wa chini ya miaka mitatu, ili kubaini kama wana matatizo ya usonji na kuwapeleka hospitalini ili wapatiwe matibabu.

Mtaalamu wa magonjwa ya watoto katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Raymond Mgeni, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu tatizo la usonji.

Alisema usonji ni miongoni mwa magonjwa ya akili kwa watoto ambayo yanaweza yakatambulika mapema endapo wazazi watawachunguza mapema watoto wao na kwamba ni moja kati ya matatizo ambayo yanarekebishika.

Alisema moja kati ya dalili ambazo watoto wenye usonji huwa wanakuwa nazo ni pamoja na kufanya matukio ya kujirudiarudia pamoja na kutopenda kuchangamana na watoto wenzao.

# Waishauri serikali kuandaa maeneo ya ukusanyaji wa mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya Shirika la Ndege nchini (ATCL) kutangaza kuwa inatarajia kupokea ndege mpya ya mizigo mwezi ujao, baadhi ya wadau wa usafirishaji wa mizigo kwa njia ya anga wameiomba serikali kuandaa maeneo maalumu ya kukusanyia mazao ya wakulima ili kurahisisha usafirishaji.

Wadau hao wamesema serikali ikiandaa utaratibu huo itawasaidia hata wakulima wadogo walioko vijijini kusafirisha mazao yao kwa kutumia usafiri huo, hivyo kuongeza thamani ya mazao na kufanya sekta ya kilimo kuongeza kiwango cha uchangiaji kwenye pato la taifa.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha pamoja kati ya wadau na maofisa wa ATCL kilichokuwa na lengo la kuwaandaa wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuchangamkia fursa ya ujio wa ndege hiyo.

Mmoja wa wadau hao, Elizabeth Mwakatobe, alisema moja kati ya mazao ya wakulima ambayo yatakuwa yanasafirishwa kwa kutumia ndege hiyo ni matunda na mboga ambayo ni mazao yanayoharibika haraka.

Alisema ili kuepuka mazao hayo kuharibika serikali ya mkoa kwa kushirikiana na TCCIA kuandaa eneo ambalo wakulima watakuwa wanakusanya mazao hayo na kuyaandaa kwa ajili ya kusafirisha.

Alisema kama usafiri huo utakuwa kwa ajili ya wafanyabiashara wakubwa pekee kuna uwezekano tija yake ikawa ndogo kwa wakulima wa kawaida.

"Serikali inaweza ikaandaa vyumba maalumu vyenye baridi (Cold rooms) kwa ajili ya wakulima kuhifadhi mazao yao kabla ya kuyasafirisha ili yasiharibike, tusipofanya hivyo hii ndege haitawasaidia wakulima wetu," alisema Elizabeth.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu alisema ndege hiyo itasaidia kupunguza upotevu wa mazao ya wakulima ambayo yamekuwa yakioza kabla hayajafika sokoni.

Alisema Wilaya ya Rungwe ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa maparachichi, ndizi na mazao matunda na mboga ambayo yatakuwa yanasafirishwa kwa kutumia ndege hiyo.

Aliwataka wakulima wa wilaya hiyo kujiandaa kunufaika na ujio wa ndege hiyo kwa kuongeza uzalishaji na kuhakikisha wanazalisha kwa viwango ambavyo vitakubalika kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

"Wakulima wetu wamekuwa wakiingia hasara wakati mwingine baada ya kukosa soko la mazao yao, mazao hayo yamekuwa yakioza kwa sababu ya kuchelewa kusafirishwa lakini ujio wa ndege hii utasaidia kupunguza upotevu huo," alisema Haniu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, alisema ndege hiyo itasaidia kulitambulisha zao la kakao linalozalishwa katika wilaya hiyo kwenye soko la dunia.

Alisema wakulima wamekuwa wakizalisha zao hilo kwa wingi lakini wanategemea wanunuzi wanaowafuata wilayani humo na kwamba ndege hiyo itasaidia kuwafikia na wateja wengine walioko kwenye maeneo mengine.

Mkaguzi wa ndani wa ATCL, Cassim Mambo, alisema kwa sasa shirika hilo kwa kushirikiana na mamlaka zingine wameanza mikakati ya kuboresha miundombinu kwenye viwanja vya ndege kwa ajili ya kusaidia usafirishaji wa mizigo hiyo.

Alisema moja ya maeneo muhimu ambayo yanatakiwa kuandaliwa ni pamoja na maghala yenye baridi kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya wakulima kabla hayajasafirishwa.

Alisema mazao hayo yanatakiwa kusafirishwa yakiwa yana ubora lakini endapo hakutakuwa na miundombinu hiyo kuna hatari baadhi ya mazao hayo yakawa yanapoteza ubora.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka wadau kujiandaa kuhakikisha ndege hiyo inajaa mizigo kila siku.

Alisema endapo wafanyabiashara watakuwa wanaijaza kila siku kuna uwezekano hata uongozi wa shirika hilo ukaongeza safari za kwenda katika mkoa huo.

# Polisi yaonya vijana matumizi mitandao ya kijamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limewataka vijana kutumia vizuri mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutafuta fursa za maendeleo na siyo kudhalilisha au kutumia kufanyia uhalifu.

Mkuu wa Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Kimtandao kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar, Issa Muhammed Salum, alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu matumizi sahihi ya utumiaji wa mitandao ya kijamii.

Salum alisema utumiaji mbaya wa mitandao ya kijamii huongeza vitendo vya udhalilishaji mitandaoni.

Alisema hali ya ukatili na udhalilishaji kupitia teknolojia ya kimtandao siyo nzuri kwa sababu watumiaji wengi hawajui sheria, kanuni na taratibu za matumizi salama ya kimtandao hiyo.

Hivyo, aliitaka jamii hasa wanawake kuacha kurusha picha zao za faragha katika mitandao ya kijamii ili kuepukana na udhalilishaji wa kimtandao.

"Baadhi ya wanawake wanatuma picha katika mitandao ya kijamii hata wakiwa katika sehemu za faragha picha ambazo wahalifu wa mitandao wanauwezo wa kuzitumia vibaya na kuwadhalilisha,"alisema.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi linaendelea kupambana kudhibiti matukio hayo ili kuhakikisha uwepo wa matumizi sahihi ya teknolojia.

Aidha, alisema Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 Kifungu cha 23 ni kosa kwa mtu yoyote kuanzisha au kutuma mawasiliano ya kielektroniki kwenda kwa mtu yoyote kwa lengo la kulazimisha, kutisha, kunyanyasa au kusababisha maudhui ya kihisia kwa mtu mwingine.

''Sheria hiyo adhabu yake kwa atakayekiuka atakuwa ametenda kosa na atawajibika iwapo atatiwa hatiani kulipa faini ya Sh.milioni tano au kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela," alisema.

Dk. Sikujua Omar, kutoka Chuo Kikuu Zanzibar alisema sheria za mitandao zinakataza matumizi mabaya ya mitandao, hivyo ni jukumu la TCRA kuzidi kuimarisha ulinzi.

Mkurugenzi wa Taasisi ya ZYF, Maulid Suleiman Juma, aliwataka wazazi na walezi kuwa na udhibiti wa matumizi ya simu kwa watoto wao ili kuwakinga na madhara ya teknolojia.

Alisema baadhi ya wazazi na walezi huachia simu watoto na kuangalia vitu ambavyo havihusu jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao.

Aidha, aliwataka vijana kutumia teknolojia kwa ajili ya kuongeza fursa za ajira na mambo ya kimaendeleo na siyo kwa matumizi mabaya yanayoweza kuwaingia katika matatizo.

## Washauriwa kula vyakula vya asili kujikinga na utapiamlo

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wametakiwa kujikinga na maradhi yasiyoambukiza kuondokana na ulaji wa vyakula visivyokuwa vya asili ili kujikinga na utapiamlo.

Ofisa Lishe kutoka PELUM, Beatrice Saria, alitoa rai hiyo wakati wa mafunzo ya lishe bora na ulaji sahihi, kusema kuwa lazima jamii iwe na mwamko kuhusu lishe.

Beatrice alisema juhudi kubwa zinazofanywa na serikali zimefanikiwa kupiga vita tatizo la utapiamlo kwa kiwango kikubwa, kwamba kwa mwaka 1999 zaidi ya asilimia 48 ya watoto wenye udumavu waliripotiwa.

Alisema ripoti ya Wizara ya Afya mwaka jana inaonyesha tatizo hilo limepungua na kufikia asilimia 30.

Beatrice alisema elimu inayotolewa kwa jamii kuhusu lishe bora imesaidia kupunguza kiwango cha watoto wenye utapiamlo na udumavu.

"Naiomba jamii izingatie ulaji bora unaotakiwa kwa ajili ya mahitaji ya mwili kutokana na kuepusha athari zikiwamo za magonjwa yasiyoambukiza yasiweze kutokea katika mwili," alisema Beatrice.

Ofisa Mtetezi kutoka Taasisi ya PELUM, Pessa Kussaga, alisema faida za kula mlo kamili huwezesha mwili kupata virutubisho vyote vinavyohitaji, usalama na afya pamoja na kupata nguvu za kufanya shughuli mbalimbali za kuboresha kinga ya mwili dhidi ya maradhi.

Pessa alieleza kuwa tatizo la jamii ni kula vyakula vyenye wanga na vinavyokaangwa jambo ambalo linasababisha maradhi yasiyoambukiza, hivyo aliishauri jamii kutumia vyakula vya asili kwa kulinda afya ili kuepukana na tatizo la maradhi.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Sabahi Bakari Hassan, alisema mafunzo hayo waliyopewa watayafikisha kwa wengine ili jamii iweze kuelimika.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na PELUM kwa Kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani (FAO).



Diwani wa Kata ya Kilungule iliyoko Mbagala jijini Dar es Salaam, Saidi Fela maarufu 'Mkubwa na Wanawe' (mwenye kofia katikati), akiwa pamoja na viongozi wa Taasisi ya Alliance Club inayojihusisha na upandaji wa miti kwenye maeneo yenye uhitaji juzi, baada ya kumaliza kupanda miti kwenye Shule ya Sekondari Kilungule. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Mawakili wataja dawa kuondoa migogoro ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAWAKILI Zanzibar wamesema ili kupunguza migogoro ya ardhi katika jamii ni vyema Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kuwashirikisha masheha katika hatua za mauzo ili kuepusha migogoro.

Rais wa Mawakili Zanzibar, Slim Said Abdallah, aliyasema hayo jana katika kikao cha pamoja kati yao na Waziri wa wizara hiyo, Rahma Kassim Ali.

Wakili Masoud Hamidu Rukazibwa, alisema pamoja na kuweka katazo la masheha wasijihusishe na suala la uuzaji wa ardhi, lakini kutokana na kuwa wao ndiyo wanaojua mipaka na maeneo ya wananchi wao ni vizuri wakashirikishwa.

Alisema shida ya migogoro ya ardhi iliyopo inasababishwa na kutokuwapo na utaratibu wa kisheria katika uuzaji wa ardhi hasa kwa wananchi.

"Haiwezekani mtu anauza nyumba ya Sh. milioni 30 au zaidi halafu asiwepo mwanasheria hili ni tatizo ambalo linatakiwa kuangaliwa kwa kina," alisema.

Wakili Fatma Ngomuo alisema sheria zilizopo za masuala ya ardhi nyingi zimepitwa na wakati, kwamba zinahitaji kufanyiwa mapitio.

Waziri wa Ardhi, Rahma Kassim Ali, alisema suala la uadilifu na uwepo wa ushirikiano mzuri ni nyenzo kuu ya kuondoa migogoro ya ardhi.Alisema ni wajibu wa kila mmoja kushirikiana katika kuondosha migogoro hasa ya uuzaji wa ardhi.

# Rufani kesi meno tembo yatupwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha imetupilia mbali rufani iliyowasilishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na kuamuru wajibu rufani waliotiwa hatiani kwa kukutwa na meno ya tembo waachiwe huru.

Walioachiwa huru ni Nayai Saning'o na Jeremiah Simulek, baada ya kubainika kwamba mahakama ilikosea kuwatia hatiani.

Hukumu hiyo ilitolewa mbele ya Jaji Mohammed Gwae baada ya kusikiliza rufani iliyowasilishwa na DPP ya kupinga adhabu waliyopewa warufani, akidai ilitolewa kinyume cha sheria.

Wajibu maombi pia waliwasilisha rufani wakipinga kutiwa hatiani na adhabu kwa madai kwamba mahakama ilikosea.

Wajibu rufani walishtakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kwa kosa la kupatikana na nyara ya serikali kinyume cha sheria.

Ilidaiwa Desemba 7, 2016 katika Kijiji cha Kiwandani wilayani Karatu katika Mkoa wa Arusha, wajibu rufani kwa pamoja walikamatwa na vipande 10 vya meno ya tembo sawa na tembo watano waliouawa, yote yakiwa na thamani ya Sh. milioni 163 mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa wanyamapori.

Machi 25, 2022, Mahakama iliwatia hatiani washtakiwa na kutakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 15 au kutumikia kifungo cha miaka 20 jela.

Katika utetezi wake, mjibu rufani namba moja alikiri kukamatwa Desemba 16, 2016 katika Kitongoji cha Chonomeloka akiwa katika Kampuni ya Langai Katopi.

Inadaiwa katika utetezi, kuwa macho yake yalifungwa na shuka na kupelekwa kwenye chumba ambacho aliwakuta watu watatu.

Alidai polisi walimpiga Desemba 17, 2016, alitoa vyeti vya matibabu kama kielelezo mahakamani hapo.

Mjibu rufani wa pili alikanusha kupatikana na nyara kinyume cha sheria na kukamatwa eneo la Kiwandani, alidai alikamatwa eneo la Ilkupus.

Pia, alidai kwamba polisi walimtesa akiwa katika chumba na katika kuunga mkono utetezi wake, alitoa vyeti vya matibabu.

Kutokana na kutoridhishwa na adhabu zilizotolewa na mahakama dhidi ya walalamikiwa, DPP aliwasilisha rufani na wakati huo huo wajibu rufani wakawasilisha rufani pia.

DPP katika sababu za rufani alidai mahakama ya chini ilikosea kutoa hukumu kila mmoja kulipa faini ya Sh. milioni 15 kinyume na Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori, Namba 5 ya mwaka 2009.

Wajibu rufani katika rufani yao walikuwa na sababu 10 ikiwamo Hakimu Mkazi alijipotosha kuwatia hatiani na kuwahukumu kwa madai kwamba kesi hiyo ilithibitishwa bila kuacha shaka licha ya mashaka yaliyojitokeza.

Inadaiwa mahakama ilikosea kupokea kielelezo cha hati ya kukamata mali, ilikosea kuzingatia ushahidi wa upande wa mashtaka uliokuwa unajichanganya, ilikosea kupuuza ushahidi uliotolewa na wajibu rufani.

Katika rufani hizo DPP akiwakilishwa na Wakili wa Serikali, Alice Mtenga, huku wajibu rufani waliwakilishwa na Wakili John Kivuyo.

Jaji Gwae baada ya kupitia rufani hizo alisema mahakama inaona hakuna ushahidi wa kuwatia hatiani wajibu rufani na kwamba ushahidi wa upande wa mashtaka una mkanganyiko.

Alisema upande wa mashtaka walishindwa kumuita mahakamani mpelelezi wa kesi hiyo wakati ushahidi wake ni muhimu.

Pia katika hati ya kukamata mali kuna mkanganyiko wa idadi ya watuhumiwa, kutokana na sababu hizo na nyingine Mahakama ilikubali rufani iliyowasilishwa na wajibu maombi na kuitupa rufani ya DPP.

Kutokana na hali hiyo, Jaji Gwae alisema: "Hukumu inafutwa, hatia na adhabu vinaondolewa na mahakama inaamuru wajibu rufani watolewe gerezani mara moja isipokuwa kama kuna sababu nyingine yoyote ya kuwafanya waendelee kuwapo gerezani."




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (katikati), akiwa na viongozi mbalimbali kwenye kongamano la miaka miwili ya mafanikio ya utawala wa Rais Samia mkoani Shinyanga, (kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, akifuatiwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Mabala Mlolwa, (kulia) ni Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, akifuatiwa na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Alliance Club yapanda miti kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Halfani Chusi**

TAASISI ya Alliance Club, inayojihusisha na upandaji wa miti imepanda miti 250 katika Shule ya Sekondari Kilungule iliyopo Mbagala jijini Dar es Salaam, ikiwa ni mwendelezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Sabira Salim, alisema walipoombwa kupeleka huduma kwenye shule hiyo hawakusita kwa kuwa wanatambua umuhimu wa miti kwenye maendeleo ya watu.

Salim alisema lengo lao wanafunzi watakapoanza kuitumia shule hiyo wakute miti tayari imekuwa mikubwa ili iweze kuwasaidia kupata hewa safi na kufurahia maisha ya shule.

"Mbali na kupanda miti pia taasisi yetu inatoa msaada kwenye mambo mbalimbali ikiwamo matatizo ya macho, mazingira, wagonjwa wa kisukari, saratani, wenye tatizo la njaa," alisema.

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Aziza Lubembela, aliishukuru taasisi hiyo kwa kupeleka huduma hiyo kwenye shule yake, akiahidi kushirikiana na wanafunzi kuitunza kwa kutumia mfumo wa kumkabidhi kila mwanafunzi mti mmoja kwa ajili ya uangalizi.

"Ujio wa taasisi hii kwenye shule yetu kwetu ni faraja kubwa kwa sababu eneo hili ni kame halina mti halina chochote wameletea miti ya aina mbalimbali ipo ya dawa, kivuli na matunda na tumepanda miti zaidi ya 250.

"Kuna michungwa, miashoki, mistaferi midodoma ambayo huwa inakuwa ya kijani mwaka mzima, lakini pia suala hili litaleta tija kwenye kata yetu ya Kilungule".

Diwani wa Kata ya Kilungule, Said Fela aliwataka walimu na wanafunzi shuleni hapo kuitunza miti hiyo, akikumbusha kuwa miongoni mwa mikakati ya serikali ni kupanda miti kwa wingi.

Mratibu wa taasisi inayojihusisha na upandaji miti na usafishaji wa mazingira (TCCI), Seleman Mang'uru, alisema dhumuni la mradi huo ni kuwapa uwezo wanafunzi kutambua umuhimu wa miti na uhusiano wake kwenye mabadiliko ya tabianchi.

# UVCCM vyuoni watakiwa kutangaza mafanikio ya Rais

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa kupitia Mkoa wa Morogoro, Jonas Nkya, amelitaka kundi la vijana wa vyuo vya kati na vyuo vikuu wa Umoja wa Vijana (UVCCM) Seneti ya Morogoro, kuacha kusubiri kusemewa na viongozi wa upinzani jinsi Rais Dk, Samia Suluhu Hassan anavyotekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, wakati wenye jukumu hilo ni wao kuonyesha kwa mifano na vitendo utekelezaji wa ilani hiyo.

"Wapo baadhi ya viongozi wa upinzani wanaeleza kuridhishwa na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati na kuweka demokrasia ya uhuru wa kujieleza uliofanywa na Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake kifupi, lakini nyie vijana wa CCM hamuyasemi hayo," alisema Nkya.

Nkya alisema hayo wakati wa kongamano lililoshirikisha wanavyuo wa vyuo vya kati na vyuo vikuu vilivyopo Morogoro, kumpongeza Rais Dk. Samia kwa ajili ya kutimiza miaka miwili ya utekelezaji wa Ilani ya chama hicho na kuzindua tawi jipya la Umoja wa Vijana (UVCCM) katika Chuo cha Ualimu cha Morogoro (MOTCO).

Alisema anashangazwa na kundi hilo la vijana kukaa kimya kuelezea mafanikio yaliyopatikana chini ya Rais Samia katika kipindi chake cha miaka miwili katika sekta mbalimbali ikiwamo ya elimu, afya, miundombinu na uendelezaji wa miradi mikubwa mpaka wasemewe na wapinzani.

"Mfano mkubwa katika sekta ya elimu ya juu nyie kundi la vyuo vikuu Rais Dk. Samia amewaongezea boom na ufadhili tena bila maandamano aliamua yeye mwenyewe na akawaita viongozi wa vyuo vikuu vya wanafunzi nchini na kuwaeleza, hivyo mnapaswa kuyasemea mazuri," alisema Nkya.

Nkya aliwaomba wanavyuo wa CCM kuwa mstari wa mbele kuelezea kwenye majukwaa na mitandao ya kijamii utekelezaji wa miradi mikubwa iliyofanywa na Rais Samia katika kipindi chake kifupi cha miaka miwili ya uongozi.

Kuhusu demokrasia nchini, Nkya alisema Rais Dk. Samia amekuwa mmoja wa viongozi msikivu wa makundi yote bila kuangalia chama ikiwamo sifa mojawapo ya kuruhusu kukosolewa kwa serikali yake ili iweze kujisahahisha hatua ambayo imerudisha imani kwa viongozi wa vyama vya upinzani.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM mkoa wa Mkoa wa Morogoro, Juliana Mwenda, alitaka kundi hilo kuacha kuiga mila nje vinazohamasisha mapenzi ya jinsi moja na kuwa mstari wa mbele kupinga mila hizo.

"Mmomonyoko wa maadili umeanza kujitokeza wapo watoto wa darasa la nne wameanza kujua mambo makubwa kuliko umri wao na hii inachangiwa na kuiga mila za kutoka nje sasa naombeni nyie vijana wa vyuo vikuu mnajielewa huo sio utamaduni wetu kabisa tupige vita hizo mila za nje," alisema Mwenda.

Awali, Kaimu Katibu wa UVCCM Mkoa wa Morogoro, Sabrina Juma, alitaka kundi hilo kuacha kuvaa sare za chama pekee badala yake watoe majibu ya utekelezaji uliofanywa kupitia ilani ya chama hicho.

HABARI KIMATAIFA

# Vikosi Russia vyabadili mwelekeo Bakhmut

**MOSCOW,** Russia

WIZARA ya Ulinzi ya Uingereza imesema Russia imebadili mwelekeo wake kiutendaji kutoka kwenye mji wa Bakhmut uliopo jimbo la Donbas na kwenda maeneo mengine ya kaskazini na kusini mwa Ukraine.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na wizara hiyo, pamoja na mkuu wa jeshi la Ukraine, Valerii Zaluzhnyi, mashambulizi ya Russia huko Bakhmut yamekwama na wanajeshi wa Ukraine wamezidi kujiimarisha.

**Sheria inapaswa kutungwa itakayoka-taza shughuli za aina yoyote za ICC kwenye eneo la nchi yetu.**

Aidha, inaelezwa kuwa vikosi vya Russia vinaelekezea juhudi kwenye mji wa Avdiivka, kusini mwa Bakhmut na Kremina Svatove, eneo la kaskazini.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa Russia inaonekana kurejea kwenye nafasi ya ulinzi zaidi baada ya juhudi zao za mashambulizi yaliyoanza Januari, kushindikana.

Taarifa ya wizara ya ulinzi ya Ukraine, ilisema jaribio la Russia kuuteka mji wa Bakhmut limeshindwa kutokana na msuguano uliozidishwa na mzozo wa ndani kati ya wanajeshi wa Russia na wapiganaji wa kampuni binafsi ya kijeshi ya Wagner ambao wote wanahusika kusambaza wapiganaji kwenye eneo hilo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa sehemu inayoizunguka Bakhmut bado ni moja ya maeneo magumu zaidi katika uwanja wa mapambano, huku Uingereza ikisema inatambua kuwa Ukraine pia imepata majeruhi wengi kutokana na mapigano ya Bakhmut.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alisema mashambulizi yanayotarajiwa dhidi ya vikosi vya Russia hayawezi kutokea sasa kwasababu nchi hiyo haina silaha, vifaa wala risasi.

Naye Spika wa Bunge la Russia, Vyacheslav Volodin, alipendekeza kupigwa marufuku shughuli za Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu, ICC nchini humo.

Volodin, ambaye ni mshirika wa Rais wa Russia Vladmir Putin, alitoa matamshi hayo baada ya mahakama hiyo kutoa waranti ya kukamatwa Putin kwa madai ya kuhusika na uhalifu wa kivita, kutokana na kuwapeleka Russia mamia ya watoto kutoka Ukraine.

"Sheria inapaswa kutungwa itakayokataza shughuli za aina yoyote za ICC kwenye eneo la nchi yetu," alisisitiza Volodin.

Pia alibainisha kuwa mtu yoyote nchini humo atakayeisaidia au kuiunga mkono mahakama ya ICC ataadhibiwa.

Volodin, alidokeza kwamba Marekani ilitunga sheria ya kuwazuia raia wake kuhukumiwa na mahakama hiyo, na kwamba Russia inapaswa kufanya hivyo hivyo. **DW**

## Lebanon yaamka na majira mawili tofauti

**BEIRUT,** Lebanon

WANANCHI nchini Lebanon wameamka jana wakiwa na majira mawili ya nyakati yanayopingana, huku kukiwa na mzozo kati ya viongozi wa kisiasa na kidini kuhusu ni wakati gani saa zinapaswa kurudishwa ama kusogezwa mbele.

Waziri Mkuu wa Muda, Najib Mikati, alitangaza kuwa mabadiliko yataanza mwishoni mwa mwezi wa Ramadhani mwezi ujao ili kuruhusu Waislamu kufungua swaumu ya kila siku saa 12, huku viongozi wa Kikristo wakisema watabadilisha saa kuanzia jana.

Mzozo huo unaonyesha mgawanyiko mkubwa katika nchi hiyo baada ya vikundi vya Wakristo na Waislamu kutajwa kuwa vilianzisha vita vya wenyewe kwa wenyewe mwishoni mwa miaka ya 1970 na 1980, na kwamba nafasi za kisiasa hugawanyika miongoni mwa vikundi hivyo. Inaelezwa kuwa nchini humo mwezi mtukufu wa Kiislamu ulianza Machi 22 ukitarajiwa kuisha Aprili 21, mwaka huu ikiwa muda utabaki bila kubadilika, na kwamba Waislamu watafuturu saa 12 jioni badala ya saa moja ya sasa nchini Lebanon, wakati jua linapozama.

Hata hivyo, Kanisa la Christian Maronite nchini Lebanon lenye ushawishi mkubwa, lilisema kwamba litapuuza uamuzi huo, na kuita wa kushangaza, huku mashirika kadhaa makubwa ya nchini humo pia yakitajwa kuamua kupuuza.

Inaelezwa kuwa vituo viwili vya habari, LBCI na MTV, vilisogeza saa zao mbele jana, huku Shirika la Ndege la Mashariki ya Kati, ambalo ni Shirika la Ndege la Kitaifa, lenyewe lilisema saa zake na vifaa vingine vitasalia kufuata majira ya baridi lakini saa zake za safari za ndege zitarekebishwa ili kuepuka kutatiza ratiba za kimataifa.

Vile vile, inaelezwa kuwa kulikuwa na mkanganyiko pia kwa watumiaji wa simu za rununu na vifaa vingine vya kielektroniki ambavyo hubadilika kiotomatiki hadi wakati wa marekebisho ya saa ya mchana, kwani waendeshaji wengi hawakuarifiwa kucheleweshwa kwa wakati. **BBC**



Baadhi ya wananchi wakiopoa vitu kwenye vifusi baada ya makazi yao kuharibiwa na kimbunga kilichopiga mwishoni mwa wiki iliyopita katika Jimbo la Massissippi kusini mwa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

## Watu 23 wauawa kutokana na kimbunga Marekani

**MISSISSIPPI,** Marekani

TAKRIBANI watu 23 wametajwa kuuawa na mamia ya makazi kuharibiwa kutokana na vimbunga vikali vilivyokumba katika jimbo la Massissippi kusini mwa Marekani.

Inaelezwa kuwa vimbunga hivyo vilikumba eneo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita, na kuacha hali mbaya katika mji wa mashambani ambao meya alitangaza kuwa haupo baada ya kuigwa na kimbunga hicho.

Idara ya kusimamia dharura ya Mississippi, ilisema katika ujumbe wa Twitter kwamba timu za utafutaji na uokoaji kutoka kwa mashirika ya ndani na serikali zilitumwa kuwasaidia walioathiriwa na vimbunga hivyo.

Idara hiyo ilithibitisha kuwa takribani watu 23 wamekufa, wanne hawajapatikana na kadhaa wamejeruhiwa, huku ikitoa hadhari kwamba huenda idadi ya majeruhi inaweza kuongezeka.

Idara ya taifa ya hali ya hewa ilithibitisha kuwa kimbunga kilisababisha uharibifu takriban kilomita 96 kaskazini mashariki mwa Jackson, Mississippi.

Aidha, inaelezwa kuwa miji ya Silver City na Rolling Fork iliripoti uharibifu, huku kimbunga kikisonga kaskazini mashariki kwa kasi ya kilomita 113 kwa saa bila kupunguza kasi kuelekea Alabama pamoja na miji ya Winona na Amory, hadi usiku. **VOA**

## Rwanda kuchagua rais na wabunge pamoja

**KIGALI,** Rwanda

BARAZA la Mawaziri la Rwanda kupitia ofisi ya waziri mkuu limesema kwamba limeamua kuoanisha tarehe za uchaguzi wa rais na wabunge nchini humo.

Katika mkutano wa baraza hilo uliofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita na kuongozwa na Rais Paul Kagame, mawaziri walipitisha pendekezo lake la kurekebisha katiba ili kuruhusu kufanyika pamoja kwa chaguzi hizo.

Aidha, inaelezwa kuwa uchaguzi mkuu wa taifa hilo, sasa unatarajiwa kufanyika Agosti mwaka huu, na kwamba awali ulipangwa kufanyika uchaguzi wa rais pekee.

Ilibainishwa kuwa kufanya hivyo kungechelewesha uchaguzi wa wabunge hadi Septemba mwaka huu.

Hatua hiyo inayosubiri kupitishwa na bunge ilitangazwa sambamba na ile ya kuachiliwa huru kwa mkosoaji wa Rais Kagame, Paul Rusesabagina aliyekuwa amehukumiwa kifungo cha miaka 25 jela kwa makosa ya ugaidi. **DW**

HABARI MICHEZO

# WASHINDI KAMPENI NBC KUPEWA TIKETI ZA LIGI KUU

Na Joseph Mwendapole

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imetangaza uzinduzi wa Kampeni ya Mkeka wa Ushindi na ATM za NBC inayolenga kuwapa watumiaji wa ATM za NBC nafasi ya kujishindia zawadi na kuweza kuwa sehemu ya kufurahia udhamini wa benki hiyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Zawadi hizo ni pamoja na tiketi za kushuhudia mechi za Ligi Kuu ya NBC, jezi, na zawadi nyingine kemkem.**

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika katika Tawi Benki la NBC la Mlimani City mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa NBC, David Raymond, alisema, kampeni hiyo inalenga kuhamasisha wateja wa benki hiyo na wasio wateja wao kutumia mashine za ATM za NBC kufanya miamala yao.

Alisema wateja ambao watatumia kadi zao za ATM kufanya miamala mbalimbali katika kipindi cha kampeni watapata nafasi ya kushinda zawadi za kusisimua, ikiwa ni pamoja na tiketi za kushuhudia Ligi ya Kuu ya NBC, jezi na zawadi nyingine kemkem.

"Tunayo furaha kuzindua Kampeni hii ya Mkeka wa Ushindi na ATM za NBC, ambayo inawazawadia watumiaji wote wa ATM za NBC ikiwa ni wateja na wasio wateja wa NBC, tunaelewa umuhimu wa urahisi katika huduma za benki, tunazidi kusogeza huduma za kibenki karibu zaidi na wateja kwa kuongeza ATM mpya kwenye maeneo mbalimbali nchini," alisema.

Aidha, alisema watumiaji wa ATM za NBC wanaweza kuweka pesa kwenye akaunti yoyote ya NBC kupitia ATM zilizopo kwenye matawi yake nchi nzima.

"Pia wale wasiokuwa na akaunti yoyote wanaotumiwa fedha kwa kutumia huduma ya NBC Cash Popote, wanaweza kutoa pesa hizo kwenye ATM yoyote ya NBC. Wote walio na kadi za VISA, Union Pay na Mastercard wanaweza kutumia ATM za NBC kutoa pesa," alisema na kuongeza kuwa makundi yote haya yanayo nafasi sawa ya kujishindia zawadi hizo katika kampeni hiyo.

"Tunaamini kuwa watumiaji wa ATM za NBC wataendelea kufurahia huduma zetu, tunawakaribisha wote watumie ATM za NBC," alisema.

Kwa upande wa Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidijitali wa Benki ya NBC, Ulrik Tobias, aliongeza kuwa zawadi hizo zitakuwa ni za papo kwa papo, pale mteja akifanya muamala wake kwa kutumia ATM ya NBC atapata kujua kuwa ameshinda zawadi gani kwa kuangalia nyuma ya risiti ya muamala wake.

"Sisi kama Benki ya NBC, daima tunawaweka wateja wetu karibu na kuhakikisha wanafurahia huduma zetu wakati wowote na popote. Kampeni yetu ya Mkeka wa Ushindi na ATM za NBC Tunafurahi kuwapa wateja wetu nafasi ya kushinda tiketi za kuona Ligi Kuu, jezi, na vitu vingine vya kumbukumbu ya Ligi ya NBC. Tunatumai kuwa kampeni hii itaimarisha zaidi uhusiano wetu na wateja wetu pamoja na watumiaji wote wa ATM zetu," alisema Urlik.




Meneja wa Tawi Benki ya NBC la Mlimani City, Lilian Mutalemwa (kushoto), akitoa zawadi ya mpira kwa Rehema Mushi, ambaye ni mshindi wa Mkeka wa Ushindi na ATM za NBC, inayolenga kuwapa watumiaji nafasi ya kujishindia zawadi mbalimbali. Utoaji wa zawadi hiyo ulifanyika mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Biashara yafifisha matumaini ya kurejea*

Na Adam Fungamwango

KIPIGO cha mabao 3-2 ilichokipata juzi dhidi ya Kitayosce, kilififisha ndoto za Biashara United kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Biashara United ambayo ilishuka daraja msimu uliopita iliambulia kipigo hicho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora na kuifanya kushika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi ya Championship, ikiwafanya wapinzani wao kukaa kwenye nafasi ya pili wakiwa na pointi 49.

Timu hiyo ambayo msimu uliopita ilicheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, ina pointi 23, ikipoteza kabisa matumanini ya kurejea Ligi Kuu kwani imecheza mechi tatu mfululizo bila kushinda, ikitoka suluhu dhidi ya Mbuni, akachapwa mabao 2-1 dhidi ya Mashujaa, kabla ya kukutana na kipigo kingine juzi.

Wakati Biashara ikipoteza matumaini hayo, ni mechi chache tu zimebakia kabla ya JKT Tanzania haijatangazwa kurejea Ligi Kuu, baada ya juzi kushinda kwa mara nyingine tena bao 1-0 dhidi ya Transit Camp, mechi ikichezwa Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, kwa bao pekee lililofungwa na Martin Kiggi.

Ni ushindi unaoifanya kufikisha pointi 56 ikiendelea kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, na kuonekana hakuna tena wa kuizuia kurejea kwenye Ligi Kuu msimu ujao, baada ya kuteremka msimu wa 2020/21.

Katika matokeo mengine ya ligi hiyo juzi, timu ya Fountain Gate ililazimishwa suluhu dhidi ya Pan African, Uwanja wa CCM Gairo Morogoro, Mashujaa ikaichapa Copco bao 1-0, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, African Sports ikalazimishwa suluhu nyumbani Mkwakwani dhidi ya KenGold na Green Warriors ikabamizwa mabao 2-1 nyumbani Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Pamba FC.

## Kabaddi yabaini vipaji vingi nchini

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa Chama cha Mchezo wa Kabaddi Tanzania, umesema umefurahishwa na viwango vilivyooneshwa na wachezaji wa timu mbalimbali kwenye kilele cha kuadhimisha Siku ya Kabaddi Duniani, ambayo kitaifa ilifanyika katika Kituo cha Utamaduni Ubalozi wa India Masaki jijini Dar es Salaam hapo juzi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Abdallah Nyoni, alisema amebaini vipaji vingi kupitia tukio hilo lililoshirikisha wachezaji kutoka shule za sekondari, vyuo pamoja na watu wazima.

"Tunashukuru tumeadhimisha kwa amani siku yetu kwa upande wa timu za mikoani wameiadhimisha kwenye mikoa yao," alisema Nyoni kuongeza kwa kuwaangukia wafadhili pamoja na wadau mbalimbali kujitokeza kwa lengo la kuchangia maendeleo ya mchezo huo.

Alizitaja timu ambazo zilipata zawadi za fedha pamoja na kombe kuwa ni Mlaleni Sekondari iliyoondoka na kombe na Sh. 60,000 kwa upande wa wanawake huku kwa upande wa wanaume zawadi kama hizo zikienda kwa timu ya Kingani Sekondari.

## Waamuzi Ligi Kuu kupigwa msasa

Na Hadija Mngwai

MWENYEKITI wa Chama cha Waamuzi Tanzania, Nassoro Hamdun, amesema wamejipanga kutoa semina tosha kwa waamuzi ili kuwaongezea ubora wao msimu ujao.

Msimu wa 2022/23 wa Ligi Kuu Bara ambao umekuwa na ushindani mkubwa huku malalamiko kwa waamuzi yakiwa yamepungua kwa kiasi fulani, unatarajiwa kufikia tamati Mei 28, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Hamdun alisema mafanikio ya ubora wa waamuzi msimu huu yametokana na umakini wa hali ya juu kuanzia Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB) na kamati ya waamuzi, hivyo wamepanga kuendeleza semina ili kuwaboresha zaidi waamuzi kuelekea msimu ujao wa 2023/24.

"Waamuzi wamekuwa bora msimu huu kutokana na umakini uliokuwapo kuanzia TFF, Bodi ya Ligi na Chama cha Waamuzi kwa kufuatilia mienendo yao ndani na nje ya uwanja ikiwa ni pamoja na kuwapa semina tosha za kuwataka wasimamie Sheria 17 za mchezo huo.

"Tumeandaa mikakati ya kuhakikisha waamuzi wetu wanakuwa bora zaidi msimu ujao na ili upate waamuzi walio bora kuchezesha soka ndani na nje ya nchi, wanatakiwa wapatiwe semina endelevu zitakazowasaidia kuwajenga ili kuwa imara," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MITROVIC ATAJWA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Fulham na Timu ya Taifa ya Serbia, Aleksandar Mitrovic, 28, alikuwa akisakwa na Manchester United kabla ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu Old Trafford kwa kumsukuma mwamuzi Chris Kavanagh. ***(Daily Star)***

### LAVIA KUNUNULIWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazohitaji kumnunua kiungo wa kati wa Southampton raia wa Ubelgiji, Romeo Lavia, 19. ***(Fabrizio Romano)***

### MODRIC KUSTAAFIA MADRID

KIUNGO Luka Modric, 37, amepuuza tetesi za kuhamia Klabu ya Saudi Arabia huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia akisema anataka kustaafia Real Madrid. ***(Mail)***

### HOJLUND LULU MAN UNITED

MANCHESTER United "wana nia ya dhati" ya kumsajili mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund, 20, ambaye anachezea Atalanta. ***(Ekstra Bladet, via Spoti Shahidi)***

### HAALAND MKATABA MPYA

MANCHESTER City iko tayari kumpa mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland, 22, mkataba mpya wenye thamani ya pauni 500,000 kwa wiki ili kuzuia nia ya Real Madrid wanaomnyatia. ***(Sun)***

### PHILLIPS ATAKIWA LEEDS

KLABU ya Leeds United ina nia ya kumsajili tena kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, 27, msimu huu wa majira ya joto licha ya kwamba alijiunga na Manchester City mwaka jana. ***(Daily Star)***

### ZEBRI KUWEKEWA NGUMU

KLABU ya Brighton haitamruhusu kocha, Roberto de Zerbi, 43, kuondoka kwenda kujiunga na Tottenham Hotspur wanaomtaka achukue mikoba ya bosi wao wa sasa, Muitaliano mwenzake Antonio Conte, 53. ***(Press)***

### TUCHEL NA MAZUNGUMZO

HAKUNA mazungumzo yaliyokuwa yamefanyika kati ya Tottenham Hotspur na Mjerumani, Thomas Tuchel, 49, kabla ya kocha huyo wa zamani wa Chelsea kuteuliwa kuwa kocha wa Bayern Munich Ijumaa iliyopita. ***(Evening Standard)***

### FERGUSON AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United pia ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, 18. ***(Football Insider)***

### WARD-PROWSE KUONDOKA

KIUNGO wa kati wa England, James Ward-Prowse, 28, bila shaka ataondoka Southampton msimu huu wa majira ya joto ikiwa watashuka daraja, huku Tottenham wakitaka kumsajili. ***(Football Insider)***

### UGARTE AVUTIA

KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na kiungo wa kati wa Sporting Lisbon, Manuel Ugarte, 21. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SHEIKH ATOA OFA MPYA KUINUNUA MAN UNITED

**Bilionea wa England, Ratcliffe naye awasilisha zabuni yake mpya, wengine kibao...**

**LONDON,** England

SHEIKH Jassim bin Hamad Al-Thani amewasilisha ofa iliyoboreshwa zaidi ya kuinunua Manchester United, vyanzo vimeiambia ESPN.

**Mmiliki huyo wa benki wa nchini Qatar alipaswa kutoa ofa yake ya pili kabla tarehe ya mwisho ya nchini England Jumatano, ikiwa ni kabla ya wazabuni wote kupewa muda wa ziada.**

Ofa ya Sheikh Jassim iliwasilishwa Ijumaa na sasa itazingatiwa na wamiliki wa sasa wa klabu hiyo familia ya Glazer.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba wazabuni hawatarajii jibu la haraka kwa matokeo yao ya hivi karibuni.

Bilionea wa England, Sir Jim Ratcliffe, Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kemikali ya INEOS, alithibitisha zabuni yake ya pili katika taarifa fupi Alhamisi.

Ilisomeka: "Jim Ratcliffe na INEOS tunaweza kuthibitisha kuwa tumewasilisha zabuni iliyorekebishwa."

Mfanyabiashara Thomas Zilliacus pia amedai kuwa amewasilisha ombi la kuchukua mikoba ya Old Trafford.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba, baada ya duru ya zabuni ya pili, familia ya Grazer inaweza kuuliza ofa ya tatu au kutaja mzabuni anayependekezwa.

Wafanyakazi wa Man United wameambiwa kutarajia "uwazi" juu ya hali ya umiliki ifikapo mwishoni mwa msimu.

Katika taarifa iliyotolewa Novemba, Glazers walisema watachunguza "njia mbadala" ambazo ni pamoja na mauzo kamili au uwekezaji wa wachache.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Glazers wanaweka chaguzi zao zote zipo wazi na kwamba idadi ya fedha pia itawekwa hadharani.


SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
IRELAND
VERSUS
FRANCE
1 | 6.67
X | 4.14
2 | 1.50

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KITUO CHA MAZOEZI CHA ARGENTINA CHAITWA MESSI



**BUENOS AIRES,** Argentina

TIMU ya Taifa ya Argentina imemtunuku Lionel Messi kwa kutwaa Kombe la Dunia kwa kukipa kituo chao cha mazoezi jina la nahodha huyo.

Casa de Ezeiza kilichopo jijini Buenos Aires, ni nyumbani kwa Timu ya Taifa ya Argentina, lakini sasa kitajulikana kama Lionel Andres Messi.

Chiqui Tapia, rais wa Chama cha Soka cha Argentina (AFA), alithibitisha habari hiyo Jumamosi, akiandika kwenye Twitter: “Tuliishi siku ya kihistoria katika Casa de Ezeiza yetu, ambayo kuanzia leo itaitwa Lionel Andres Messi, kwa heshima ya mchezaji bora wa mwaka wa Dunia.

“Nataka kuwashukuru makocha, wachezaji na wafanyakazi wote wa AFA kwa kuwa nasi.”

Messi aliiwezesha Argentina kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka jana, akifikia mafanikio ya marehemu Diego Maradona huku ‘La Albiceleste’ hao wakitwaa taji lao la tatu la dunia, na la kwanza tangu mwaka 1986.

“Kutambuliwa huku ni mojawapo ya mazuri zaidi ambayo nimewahi kupokea,” alisema Messi akiandika kwenye Instagram. “Heshima kubwa, asante sana!!!”

Messi alifunga bao la 800 katika maisha yake ya soka katika ushindi wa 2-0 kwenye mechi ya kirafiki kati ya Argentina na Panama.

Bao linalofuata la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, kwenye medani ya kimataifa litakuwa la 100 kwa nchi yake.



# Tuchel: Nina changamoto kubwa

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA mpya wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, amekiri kuwa anakabiliwa na mwanzo mgumu wa kazi yake mpya baada ya kuajiriwa kwa mshangao Ijumaa kuchukua nafasi ya Julian Nagelsmann.

Tuchel anaingia moja kwa moja kwenye michezo muhimu, akianza na wapinzani wa taji la Ujerumani -- na klabu yake ya zamani, Borussia Dortmund hapo Aprili Mosi, mwaka huu.

“Changamoto haiwezi kuwa kubwa zaidi,” alisema Tuchel.

Siku kumi baadaye, Bayern inacheza na Manchester City katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kutakuwa na muda mchache wa kupumzika au kufanya mazoezi ya mbinu mpya, wachezaji wengi wa Bayern kwa sasa hawapo kwani wapo na timu zao za taifa na kisha michezo saba katika siku 22 za kwanza za Aprili.

“Nilikuwa muoga katika mazungumzo ya kwanza na Bayern. Katika sekunde 30 za kwanza sikujua tulichol wa tunajadiliana au kilihu nini,” alisema Tuchel.

“Mara tu ilipobaini kuwa Bayern walinita nichukue jukumu hilo ma moja, ilinijia kwamba inaa za mara moja na Dortmun

Tuchel alisema hatua hi ilishangaza na kwamba h majuzi, Jumanne haku na mawasiliano yoyote Bayern.

Alifikiria kazi yake inay fuata itakuwa nje ya Ujer mani, aliongeza, lakini a kuwa akifuatilia msimu Bayern.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 27/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5089 | Leixoes SC U23 vs CS Maritimo U23 | 2.18 | 3.32 | 2.95 |
| 14:00 | 4445 | Crewe U23 vs Ipswich U23 | 2.70 | 3.89 | 2.12 |
| 15:15 | 3250 | Kifisias vs GS Ilioupoli | 1.13 | 6.20 | 19.63 |
| 16:00 | 2191 | Eding Sport FC vs Stade Renard | 2.25 | 2.75 | 3.42 |
| 16:00 | 3830 | Rwanda vs Benin | 2.64 | 2.96 | 2.75 |
| 16:00 | 4457 | South Sudan vs Congo | 3.22 | 2.90 | 2.35 |
| 16:00 | 4534 | Central African Republic vs Madagascar | 2.03 | 3.23 | 3.60 |
| 16:30 | 3385 | Arema vs Bali Utd Pusam | 2.61 | 3.33 | 2.34 |
| 17:00 | 1001 | FK Radnicki Sremska Mitrovica vs FK Zlatibor | 1.52 | 3.61 | 5.77 |
| 17:00 | 1253 | FK Loznica vs FK Imt Novi Beograd | 5.34 | 3.44 | 1.58 |
| 17:00 | 1691 | Burnley U23 vs Peterborough U21 | 2.79 | 3.98 | 2.04 |
| 17:00 | 2979 | Indjija vs FK Trajal | 1.81 | 2.93 | 4.63 |
| 17:00 | 3163 | Metalac vs FK Novi Sad | 2.18 | 2.93 | 3.24 |
| 17:00 | 3818 | OFK Vrsac vs FC Rad | 1.90 | 3.18 | 3.74 |
| 17:00 | 4163 | FK Radnicki Beograd vs FK Jedinstvo UB | 2.67 | 2.77 | 2.67 |
| 18:00 | 1891 | Macva Sabac vs FK Zeleznicar Pancevo | 3.84 | 2.82 | 2.02 |
| 18:00 | 3500 | Sloboda vs FK Graficar Beograd | 3.39 | 3.28 | 1.96 |
| 19:00 | 2061 | Greece vs Lithuania | 1.19 | 6.45 | 15.04 |
| 19:00 | 2791 | Niger vs Algeria | 8.62 | 4.52 | 1.35 |
| 19:00 | 3709 | Poland U21 vs Albania U21 | 1.47 | 4.04 | 5.80 |
| 19:00 | 3811 | Angola vs Ghana | 3.00 | 3.00 | 2.41 |
| 19:00 | 4661 | Guinea Bissau vs Nigeria | 4.33 | 3.28 | 1.84 |
| 19:30 | 5878 | FC Martigues vs Le Mans | 2.37 | 3.10 | 2.94 |
| 20:00 | 2091 | North Macedonia vs Faroe Islands | 1.60 | 3.71 | 6.02 |
| 20:00 | 3639 | Freiburg II vs Saarbrucken | 2.58 | 3.27 | 2.59 |
| 20:00 | 4161 | Berliner AK 07 vs BSG Chemie Leipzig | 2.36 | 3.27 | 2.70 |
| 20:00 | 5950 | IFK Norrkoping Dfk W vs Vaxjo Dff W | 1.95 | 3.65 | 2.80 |
| 20:30 | 5202 | AS Eupen U21 vs Oostende U21 | 2.46 | 3.52 | 2.45 |
| 21:00 | 1620 | Italy U21 vs Ukraine U21 | 1.51 | 3.77 | 5.79 |
| 21:00 | 2207 | CA Acassuso vs Argentino Merlo | 2.44 | 2.75 | 3.06 |
| 21:00 | 2433 | QPR U23 vs Birmingham U21 | 1.64 | 4.26 | 3.90 |
| 21:30 | 3180 | Sportivo Barracas vs Juventud Unida SM | 1.70 | 3.25 | 4.10 |
| 21:30 | 3817 | Justo Jose De Urquiza vs Claypole | 2.85 | 2.70 | 2.38 |
| 21:30 | 5926 | Pordenone vs AC Pro Sesto | 1.78 | 3.52 | 4.47 |
| 21:45 | 1019 | Austria vs Estonia | 1.22 | 6.03 | 13.99 |
| 21:45 | 1118 | Kings Langley vs Ilkeston Town FC | 2.91 | 3.58 | 2.10 |
| 21:45 | 1199 | Hungary vs Bulgaria | 1.52 | 3.87 | 6.87 |
| 21:45 | 2811 | Poland vs Albania | 1.62 | 3.70 | 5.79 |
| 21:45 | 3563 | Montenegro vs Serbia | 4.31 | 3.55 | 1.83 |
| 21:45 | 3569 | Netherlands vs Gibraltar | 1.08 | 9.90 | 26.91 |
| 21:45 | 3711 | Ireland vs France | 6.67 | 4.14 | 1.50 |
| 21:45 | 5601 | Moldova vs Czech Republic | 12.88 | 5.37 | 1.26 |
| 21:45 | 5608 | Sweden vs Azerbaijan | 1.22 | 5.84 | 14.07 |
| 22:00 | 1385 | Ethiopia vs Guinea | 4.34 | 3.17 | 1.87 |
| 22:00 | 3319 | Malaga vs Leganes | 2.71 | 2.91 | 2.66 |
| 22:00 | 3756 | Saint Vincent and the Grenadines vs Bahamas | 1.74 | 3.58 | 4.05 |
| 23:00 | 1719 | Asociacion Deportivo Cali vs CD La Equidad | 1.34 | 4.20 | 6.40 |
| 23:00 | 3389 | UTC Cajamarca vs Cusco FC | 1.97 | 3.24 | 3.39 |
| 23:00 | 5984 | Sudan vs Gabon | 3.11 | 2.85 | 2.46 |

JUMANNE - 28/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | 1 | X | 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 4510 | AD Aserri vs Municipal Turrialba | 1.49 | 4.37 | 5.00 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# STRAIKA WA FOUNTAIN GATE PRINCESS AULA KAMA OPA

Na dama Fungamwango

SIKU chache baada ya straika wa Simba Queens, Opa Clement, kupata nafasi ya kucheza soka la kulipwa nchini Uturuki katika Klabu ya Besiktas, mchezaji mwingine anayechezea Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Cynthia Musungu, raia wa Kenya naye amekwenda nchini humo kujiunga na timu hiyo.

**Taarifa zilizotolewa na Klabu ya Fountain Gate Princess, ambayo kwa sasa inaongoza Ligi Kuu ya Wanawake kwa pointi 29, Musungu ambaye naye pia alikuwa na mabao tisa kama Opa, zimeeleza amekwenda kujiunga na Klabu ya Besiktas.**

Klabu hiyo imemtakia kila la kheri mchezaji wao huyo kwenye maisha yake mapya ya soka na timu yake hiyo mpya.

Musungu amekuwa tegemeo kwa kikosi cha Foutain Gate Princess na kwa kiasi kikubwa mabao yake ndiyo yaliyofanya timu hiyo kuwa kileleni.

Huu ni mfululizo wa wachezaji wanaocheza soka nchini, hasa Ligi Kuu ya Tanzania kwa wanawake kununuliwa na kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Machi mwaka jana Opa, alikwenda Klabu ya Kayserispor Girl ya Uturuki kwa kile kilichoelezwa ni kufanya majaribio na akifanikiwa klabu hiyo ingekaa mezani na Simba kumalizaka, lakini alirejea nchini na baadaye haikufahamika kama alifuzu au la.

Hata hivyo, Klabu ya Besiktas mwaka huu ilikuja kumchukua moja kwa moja baada ya kuridhika na kiwango chake ambacho walikiona akikionyesha kwenye klabu nyingine aliyokwenda kufanyia majaribio.

Machi 2021, Simba Queens pia ilimuuza aliyekuwa nahodha wake wakati huo, Mwanahamisi Omari kwa klabu ya Shabab Atlas ya Morocco, lakini kwa sasa amerejea tena klabu ya Msimabazi kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili na anaendelea kucheza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania akisikilizia dili lingine kama litakuja.

Mchezaji mwingine ni kiungo Flavian Mawete Musolo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo aliyeichezea Simba Queens mwaka 2020 hadi 2021, ambapo aliuzwa kwa Klabu ya Adana Idmanyurduspor ya Uturuki anayoichezea hadi sasa.




Wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari za jijini Dar es Salaam, wakifanya mazoezi ya kucheza mpira wa magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Sababu Kapombe, Tshabalala kuitwa Stars*

INATOKA UKURASA 24

Hiyo inakuja siku chache tu baada ya Rais kutangaza donge nono ya Sh. milioni 500 iwapo Stars itafuzu fainali hizo.

"Mimi nasema tuendelee kumpa sapoti Rais wetu Mama Samia na hatutomwangusha, anatupa hamasa sisi wachezaji, kwa hiyo hatuhitaji kumwangusha, tutapambana, tunalipambania taifa na yeye mwenyewe akiwamo kwa sababu hamasa yake na anavyotufuatilia kila hatua ndiyo nasi inatufanya kuzidi kupigana.

"Kwenye mechi ya Jumanne ni kujipanga tu kwa sababu hatuna muda na tumebakisha siku moja tu ili tuweze kurudiana na Uganda, lakini pamoja na hayo hatutakiwi kubweteka, tujipange ili tufanye vizuri tuweze kujihakikishia tunapita kwenye kundi letu," alisema Msuva.

Kwa upande wa Samatta, alisema kwa sasa wamesahau kila kitu kuhusu mechi iliyopita, wanachoangalia ni mchezo wa kesho.

"Tunamshukuru mama ni jambo zuri na tunamwahidi hatutomwangusha, ila sisi kama wachezaji kwanza tutahakikisha tunapata ushindi kwenye mechi zote na mama kama ameamua kutuongezea motisha na morali ni jambo zuri sana, ila muhimu kwetu sote ni kuipigania nchi kwanza," alisema.

# Michezo

Jumatatu Machi 27, 2023

Nipashe




Sheikh na ofa mpya kuinunua Utd

UKURASA 21

NGUMI YA UKRAINE...




Bondia wa Ngumi za Kulipwa nchini, Karim Mandonga, akimpelekea konde mpinzani wake, Kenneth Lukyamuzi kutoka Uganda katika pambano hilo la uzani wa Super Middle kuwania mkanda wa Ubingwa wa PST, lililofanyika juzi katika Uwanja wa Kasarani jijni Nairobi, Kenya. Mandonga 'Mtu Kazi' anayetamba na ngumi yake maarufu kutoka 'Ukraine', alishinda kwa pointi. **MPIGAPICHA WETU**

## Klabu nne Ulaya zenye kiwango cha kushangaza

**LONDON,** England

MSIMU wa soka wa 2022-23 umekuwa wa kushangaza na mabadiliko yasiyotarajiwa...



HABARI UK. 11

## Yanga na rekodi ya miaka 28 robo fainali CAF



**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni siku ya kihistoria kwa wanachama, mashabiki wa Yanga baada ya klabu yao kutinga hatua ya

UKURASA 14

# Sababu kocha Stars kuwaita Tshabalala, Kapombe Taifa

## ●●● Rais TFF afunguka, Samatta, Msuva nao watia neno wakiipania Uganda kwa Mkapa kesho, huku...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KIWANGO kilichoonyeshwa na mabeki wawili wa pembeni wa Simba, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala', katika mechi dhidi ya Horoya AC wakati wakishinda 7-0 kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa wiki moja iliyopita, kimewarejesha rasmi Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Baada ya mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mualgeria Adel Amrouche, alikwenda katika chumba cha kubalishia nguo cha Simba na kuteta machache na Kapombe na Tshabalala, kabla ya Stars kwenda kushinda bao 1-0 ugenini nchini Misri dhidi ya wenyeji wa mchezo huo, Uganda (The Cranes), kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast.

Hata hivyo, kuelekea mchezo wa marudiano dhidi ya The Cranes kesho, Jumanne, Amrouche amewaita nyota hao wawili wa Simba, na mara moja wameungana na wenzao kambini kujiandaa na mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa saa1:00 usiku.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema baada ya kikosi cha Stars kurejea kocha Amrouche amewaita mabeki hao wawili kutoka Simba kwa ajili ya kuongeza nguvu katika mchezo wa kesho, Jumanne.**

Alisema awali kutoitwa kwa nyota hao ilikuwa ni matakwa ya kocha huyo na hadi sasa kuwaita kwa mara nyingi ni mapendekezo yake na halikuwa shinikizo la kiongozi yeyote.

"Asubuhi ya leo (jana) nimepokea taarifa kuwa kocha Adel amewaita mabeki wawili kutoka Klabu ya Simba Tshabalala na Kapombe, tayari wameingia kambini kuongeza nguvu kuelekea mchezo wetu dhidi ya Uganda.

"Ni mchezo muhimu na ndio karata yetu pekee ya kuingia katika fainali za Afcon, tuwashukuru serikali kwa jitihada zao za kufanikisha, tumepata kocha huyo pamoja na kutoa tiketi elfu 20,000 kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi kuisapoti Taifa Stars, dhidi ya Uganda," alisema Karia.

Aliongeza kuwa mchezo huo ni mgumu kwa sababu Uganda katika michezo mingine, Tanzania hupoteza ikiwamo michuano ya Chalenji, michuano ya vijana na CHAN.

"Safari hii tumeweza kuwafunga katika mchezo wetu wa kwanza, ushindi huo bado hatujamaliza kazi kwa sababu Uganda ni washindani wetu wametufunga katika michuano mingi kasoro Afcon, kuelekea Jumanne tunatakiwa kushinda huu mchezo muhimu ambao ni karata yetu ya kucheza fainali ya michuano hiyo," alisema Karia.

Katika hatua nyingine serikali imetoa tiketi 20,000 kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani kuishangilia Taifa Stars katika mchezo huo wa marudiano dhidi ya The Cranes.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Saidi Yakubu, alikabidhi tiketi hizo kwa Rais wa TFF ambao watakuwa na jukumu la kuwagawia Watanzania ambao wataenda uwanjani kushuhudia Taifa Stars ikivaana na Uganda kesho.

"Serikali kupitia Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan tunatamani kuona Taifa Stars inaenda kucheza fainali hizi kwa mara ya tatu, baada ya ushindi wa juzi tumeona mama ameweka ahadi ya Sh. milioni 10 kwa kila bao litakalofunga dhidi ya Uganda katika mchezo wetu wa Jumanne.

"Kitita hicho hakitahusiana na ile Sh. milioni 500 endapo timu ya Taifa itafanikiwa kufuzu fainali hizo," alisema Katibu huyo baada ya kukabidhi tiketi hizo kwa TFF.

Aliongeza kuwa katika harambee zilizofanywa na wadau mbalimbali wa soka nchini, jumla ya tiketi 31,000 za mzunguko zimekusanywa na zitagawiwa kwa utaratibu mzuri kulingana na Shirikisho la Soka litakavyoona.

Wakati huo huo, Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta na mfungaji wa bao pekee dhidi ya The Cranes, Simon Msuva, wamemshukuru Rais Samia kwa hamasa na morali kubwa anayowapa, na kumwahidi kuwa wataendelea kupeperusha vema bendera ya nchi na hawatomwangusha.

Juzi, kupitia kwa Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, Rais Samia baada ya furaha ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Uganda, aliahidi kutoa donge nono la Sh. milioni 10 kwa kila goli ambalo Stars watalifunga kuanzia mechi ya kesho na zinazofuata za kusaka tiketi ya kufuzu Afcon 2023.

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >